# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 08 | Oktoba 23, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO

# VITA VYA KENYA DRC

**Kenya imeingilia zaidi mzozo mkali dhidi ya waasi nchini Congo ambao umevuta wanajeshi wa nchi zingine za Afrika na pia mataifa yenye nguvu duniani. Huku Uganda na Rwanda zikiwa ndani ya mzozo huo, je, kujiunga kwa KDF kutajenga ama kutaharibu mahusiano katika eneo hili?**





# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.




Follow the link to subscribe
> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation
Nation
Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**8 MTEGO WA DENI LA SGR:** Kuna wasiwasi kuhusu athari za mageuzi makubwa ya Rais William Ruto katika bandari ya Mombasa kwa uhusiano na benki ya The China Exim, inayokopesha Kenya pesa nyingi za miradi ya miundomsingi kwa wakati huu.

**10 UFANISI MBALI NA NYUMBANI:** Mabadiliko katika mtindo wa kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu wa Agosti Agosti 9 yatokea katika viwango vya chini zaidi vya uwakilishi, ambako wanasiasa hutangamana na wapigakura na kuelezea ajenda zao ambazo huvunja miegemeo ya kikabila.

**13 GUMZO PESA:** Uundaji wa podcast ni biashara mpya Afrika, lakini Eli Mwendwa ameitumia kupata umaarufu na kuunda pesa kutokana na mazungumzo ya mtandaoni.



**25 MAISHA YA JEHANAMU TIGRAY:** Eneo ambalo lilikuwa kivutio cha watalii sasa limegeuka uwanja wa vita vikali vya kudhibiti sehemu yake kubwa ambayo kwa muda mrefu imeonekana kuwa muhimu katika utawala wa Ethiopia, au kihistoria iliyojulikana kama Abyssinia.

# DRC thabiti ni nzuri kwa eneo letu

Mnamo 1960, nchi iliyoitwa Belgian Congo ilipopata uhuru wake kutoka kwa utawala wa kimabavu wa kikoloni, mwanamuziki maarufu wa rhumba, Joseph 'Grand Kalle' Kabasele, alitoa wimbo Indépendance Cha Cha, uliovutia wengi barani Afrika na kuwa sawa na wimbo wa taifa nchini humo.

"Independance Cha-cha to zuwi ye! Oh Kimpwanza cha-cha tubakidi. . ."(Uhuru, cha-cha, tumeshinda! Oh, Uhuru cha-cha tumeupata), inasema mistari ya kwanza ya wimbo huo. Uliandamana na miondoko ya gitaa kutoka kwa wanamuziki wa bendi ya African Jazz, yake Grand Kalle na baadhi ya wanachama wa bendi ya Ok Jazz (baadaye TPOK Jazz) yake Franco Luambo Makiadi. Leo hii, miaka 62 baadaye, miondoko ya wimbo huo ni kumbusho la mkasa wa kihistoria wa nchi hiyo baada ya kupata uhuru wake. Awali, nchi hiyo liliitwa Zaire, lakini kwa sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Baada ya kupitia ukatili na uporaji mkubwa chini ya utawala wa kikoloni - kwanza chini ya Mfalme Leopold II wa Ubelgiji kabla ya kuchukuliwa na serikali ya Ubelgiji – nchi hiyo ilitegemea mwanzo mpya ya kujikomboa kutoka kwa minyororo hiyo. Lakini hayo hayakutimia.

Kwa zaidi ya miongo sita iliyopita, DRC imekuwa ikikumbwa na mapinduzi ya kijeshi na vita vya wenyewe kwa wenyewe, vinavyotokana na misukosuko ya kisiasa, utawala mbaya na kudorora kwa uchumi. Taswira inayojitokeza katika kitabu 'In the Footsteps of Mr Kurtz' (Katika Nyayo za Bwana Kurtz) chake Michela Wrong, kinachoelezea maovu ya dikteta ya Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu Wa Za Banga, ndiyo hiyo iliyo katika kitabu 'King Leopold's Ghost', chake Adam Hochschild, kuhusu ukatili uliotekelezwa nyakati za ukoloni.



Mike Owuor

> **Kando na uongozi wake mbaya wa kisiasa na mwingilio kutoka kwa jeshi lake dhaifu, changamoto za DRC pia zimechangiwa na kuingiliwa na mataifa ya kigeni – Amerika, Ubelgiji na Ufaransa. Katika miaka ya hivi majuzi, nchi hiyo imekuwa ikiingiliwa na mataifa jirani kama Rwanda na Uganda**

Dalili za mabadiliko halisi zilivurugika hata baada ya Laurent-Désiré Kabila kupindua serikali ya Mobutu mnamo 1997 na baadaye utawala wa mwanawe, Joseph Kabila, uliodumu kwa miaka 18. Kinaya ni kuwa, DRC ni miongoni mwa nchi zenye utajiri mkubwa wa rasilmali asilia kote duniani, hasa madini. Nchi hiyo kubwa ina watu 90 milioni.

Kando na uongozi wake mbaya wa kisiasa na mwingilio kutoka kwa jeshi lake dhaifu, changamoto za DRC pia zimechangiwa na mwingilio wa mataifa ya kigeni - Amerika, Ubelgiji na Ufaransa. Katika miaka ya hivi majuzi, nchi hiyo imekuwa ikiingiliwa na mataifa jirani kama Rwanda na Uganda. Makundi mengi ya wanamgambo ambayo yamekuwa yakiendesha shughuli zake nchini humo - hasa eneo la Mashariki - tangu uhuru, yamesababisha vifo vya maelfu ya watu, kuwaacha mamilioni bila makao na kusababisha misukosuko katika nchi inayofaa kuwa na uwezo mkubwa zaidi barani Afrika. Lakini kwa sasa, Rais Félix Tshisekedi, mwanawe aliyekuwa kiongozi wa upinzani, Etienne Tshisekedi, anataka kubadilisha hayo yote. Anatoa semi kali, huku akilijenga upya jeshi. Anaonekana kuwa na mpango mzuri wa kufufua uchumi.

Rais huyo ambaye alianza kuhudumu 2019, pia amechukua hatua muhimu sana kwa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Hata hivyo, ametaja ukosefu wa usalama kuwa changamoto kuu inayomkabili katika kuleta mageuzi kamili nchini humo.

Kurudi kwa wapiganaji wa kundi la M23 na madai mapya ya Rwanda kuhusika katika mapigano yanayoendelea DRC, ni hali inayofaa kuzua wasiwasi kwa yeyote anayetamani kuona eneo hili likistawi.

Hatua ya Rais Tshisekedi kuita Jeshi la Ulinzi Kenya (KDF) kumsaidia kurudisha amani katika baadhi ya sehemu za eneo hilo huenda ikazaa matunda. Kuhusishwa kwa vikosi vya Uganda, ambapo lengo lake kuu ni kuwakabili wanamgambo wa kundi la Allied Democratic Forces (ADF), kumezua kizungumkuti kipya cha kiusalama. Vikosi hivyo vinaonekana kutoaminika sana.

Matumaini yaliyopo ni kuwa juhudi hizo za pamoja zitaamsha tena taifa hilo kupata uhuru halisi na ufanisi.

*mowuor@ke.nationmedia.com*

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Darubini ya Wiki


Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

## Wabunge kujadili changamoto za nchi

# Bunge kuanza vikao wiki hii



Bunge la 13 mnamo Septemba 29. SILA KIPLAGAT | NATION

Bunge litaanza vikao vyake Jumanne baada ya likizo ya wiki mbili, huku wabunge walioapishwa majuzi, wakiwa tayari kuanza kazi.

Shughuli ya kwanza ya Bunge la Kitaifa na Bunge la Seneti itakuwa kupokea ripoti kutoka kwa kamati ambayo imekuwa ikipiga msasa mawaziri wateule.

Shughuli hiyo iliongozwa na Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula.

Kamati hiyo ina muda wa siku 28 tangu kikao cha kwanza kuwapiga msasa mawaziri walioteuliwa na Rais Ruto na kuwasilisha ripoti yake katika Bunge.

Bunge litajadili ripoti hiyo katika muda wa siku saba hadi Novemba 3 ili kukamilisha shughuli hiyo.

Bunge litajadili ripoti hiyo na kupiga kura kuhusu iwapo itaikubali au itaikataa.

Wabunge pia wanatarajiwa kujadili sharia ambazo zitasaidia kusuluhisha changamoto zinazokabili nchi, ikiwemo gharama ya juu ya maisha na bei ghali za petroli na stima.

## Taji la pili kwa dereva wa Uholanzi




Max Verstappen wa timu ya Red Bull akiendesha gari wakati wa mashindano ya Grand Prix, Japan, mnamo Oktoba 9. PICHA | AFP

# Verstappen, Red Bull tayari kwa Texas

Bingwa mara mbili wa dunia Max Verstappen ana kila sababu ya kusherehekea ushindi wa pili katika mashindano ya madereva wikendi hii. Lakini anapojitahidi kuvunja rekodi nyingine katika mashindano ya US Grand Prix wiki mbili baada ya ushindi katika mashindano ya Japan, bosi wake wa timu ya Red Bull, Christian Horner, atapata motisha kutokana na azma zake mbili kuu.

Azma ya kwanza ni kutetea sifa ya shirika hilo lenye makao makuu mjini Milton Keynes kukiwa na madai kuwa 'walidanganya' walipoelekea kumwezesha Max Verstappen kunyakua mataji yake mawili mtawalia ya ubingwa 2021 na 2022.

Shutuma hizo ambazo zimetia doa ufanisi wake katika siku za hivi majuzi ulijiri baada ya Red Bull kupatikana na hatia ya kukiuka kiwango rasmi kilichowekwa kuhusu bajeti ya 2021 - ambayo bado hawajafahamishwa adhabu yake, lakini iliyochochea timu moja hasimu kusema wamekuwa wakidanganya.

Azma ya pili ya Horner ni kuhakikisha timu hiyo imebakia makini na kudumisha kiwango chake ambacho kimewezesha nyota huyo kuendelea kufanya vyema tangu 2013.

## Mashirika yatahitajika kupata leseni

# Afrika Kusini kudhibiti pesa dijitali



Shirika linalosimamia masuala ya pesa Afrika Kusini limetangaza pesa dijitali kuwa bidhaa ya kifedha na kutoa nafasi ya kudhibiti kisheria mali hizo nchini humo iliyopiga hatua kubwa kiuchumi Afrika. Tangazo hilo limejiri wakati ambao taasisi za kifedha duniani zinatatizwa na jinsi ya kudhibiti pesa dijitali. Uamuzi huo wa Mamlaka ya Utendaji wa Sekta ya Kifedha (FSCA) unaamanisha mashirika ya kifedha yanayotumia pesa dijitali yatahitajika kupata leseni mwaka ujao. "Haiwezekani kwa mashirika kuendesha shughuli za kifedha nje ya mfumo wa sheria," akasema Kamishna wa FSCA, Unathi Kamlanag.

## Wafuasi wa Franck tayari kwa uchaguzi 2025

# Mwanawe Biya ataka urais Cameroon



Katika wiki chache zijazo, Paul Biya atasherehekea miaka 40 akiwa rais wa Cameroon. Kiongozi huyo wa miaka 89 hajaonyesha dalili zozote za kutaka kuachilia wadhifa huo, ingawa wakosoaji wake wanadai huwa anatumia muda wake mwingi Ulaya, huku mapigano katika maeneo ya nchi hiyo yakiongezeka. Hata hivyo, mjadala mkali unaendelea nchini Cameroon kuhusu ni nani anafaa kumrithi Paul Biya.

Miongoni mwa wanaotazamiwa kugombea urais katika uchaguzi huo wa 2025 ni Franck Biya, mwanawe rais huyo. Hajasema mengi kuhusu mpango wake lakini kuna makundi ambayo yanamuunga mkono.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ NI KAZI ISIYOWZEKANA KWA JESHI LA KENYA?

# JUHUDI ZA AMANI CONGO

*Jeshi la Ulinzi la Kenya liko katikati ya mzozo usioisha ambao kwa miaka mingi umevuta mataifa ya mbali ya Afrika kama Afrika Kusini na Angola; pia nchi zenye nguvu ulimwenguni kama Amerika, Ufaransa, China, Ubelgiji na Uingereza*



● Na MACHARIA GAITHO

Wanajeshi wa Kenya wako katika hatari ya kujipata katika mzozo wa moja kwa moja na waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda wanapojiunga na mpango wa amani wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta zinazosimamiwa na wanamgambo hao sehemu ya mashariki ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo.

Inadaiwa waasi hao wanaopigana na serikali ya Rais Félix Antoine Tshisekedi wanaungwa mkono na Rais Paul Kagame wa Rwanda - dai ambalo Rwanda inakanushwa.

Wataalamu wa kijeshi wanasema wanajeshi waliozoea vita wa Kagame wamekita kambi mashariki ya DRC tangu kutimuliwa kwa serikali ya marehemu Juvenal Habyarimana mnamo 1994 na kufukuzwa kwa jeshi lake kwenye mpaka.

Wanajeshi wa Kagame wa Rwanda Patriotic Front pia waliungana na wanajeshi wa wafadhili wao wakati huo, National Resistance Army ya Rais wa Uganda Yoweri Museveni, kuingia ndani ya iliyojulikana wakati huo kama Zaire, kumuondoa mamlakani dikteta aliyetawala kwa miaka mingi Mobutu Sese Seko, ambaye nafasi yake ilichukuliwa na kiongozi wa waasi, Laurent Kabila.

Tangu wakati huo, eneo la Mashariki mwa DRC, ambalo lina madini mengi, limekuwa uwanja wa wanajeshi wa Rwanda na Uganda kuchezea, ambao wamegeuka kutoka washirika wa dhati hadi maadui wakubwa.

Kuingia katika mzozo huo kama kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kunaweka Jeshi la Ulinzi la Kenya katikati ya mzozo usioisha, ambao kwa miaka mingi umevuta mataifa ya mbali ya Afrika kama Afrika Kusini na Angola; pia mataifa yenye nguvu ulimwenguni kama Amerika, Ufaransa, Ubelgiji, China na Uingereza. Kagame ametumia waasi wa M23 kukabiliana na wanamgambo waliobakia wa Interahamwe wanaochukuliwa kuwa wahusika wakuu wa mauaji ya halaiki ya 1994 nchini Rwanda.

Walibaki Mashariki mwa DRC ambako wamekuwa wakitishia serikali ya Kagame ya Rwanda Patriotic Front, na amekuwa akikabil-

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Congo: Sehemu mpya ya mapigano kwa KDF

Kutoka Uk 5

iana na vitisho hivyo kwa kuweka wanajeshi wake kwenye mpaka. Matarajio ya mwanzo ya kuwa na kikosi cha kudumisha amani yamekuwa yakizimwa katika miaka ya hivi majuzi kufuatia tafsiri tofauti kuhusu jukumu la kikosi cha pamoja cha kanda ya Afrika Mashariki na kati.

Mwanzoni ilitarajiwa kuwa Tshisekedi na Kagame wakijiunga, mambo yangekuwa rahisi. Hata hivyo, rais huyo wa DRC bado anamlaumu mwenzake wa Rwanda kwa kusaidia waasi wa M23 ambao wanashikilia maeneo yaliyo karibu na Goma na kushambulia kambi za wanajeshi wa serikali yake.

Tshisekedi anashikilia kuwa jukumu la kikosi cha kudumisha amani cha kanda ni kusaidia jeshi lake kupigana na waasi na wafadhili wao kutoka Rwanda, badala ya kudumisha amani huku suluhu ya kisiasa ikiafikiwa.

Kagame amekataa msimamo huu na hivyo basi kuchelewa kutoa wanajeshi wake katika eneo la vita.

Katika mwaka mmoja uliopita, Kenya imetekeleza wajibu muhimu wa kutafuta amani mashariki ya DRC ukiongozwa na aliyekuwa rais Uhuru Kenyatta, ambaye baada ya kuondoka ofisini mwezi jana aliombwa na mrithi wake William Ruto endeleze mpango huo ambao sasa unajulikana kama 'Mikutano ya Nairobi'.

Afisa wa cheo cha juu katika Wizara ya Mashauri ya Kigeni jijini Nairobi hata hivyo alipuuza tisho la wanajeshi wa Kenya na wa Rwanda kupigana. Alisema kutumwa kwa wanajeshi kudumisha amani na uthabiti mashariki ya DRC kuliafikiwa na nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Rwanda, ambayo alisema ilikubali kuondoa jeshi lake mashariki ya DRC na kuzingatia kulinda mpaka wake kutoka upande wake.

Uganda, Burundi na Tanzania, zote zinatoa wanajeshi kuunda kikosi cha pamoja cha Jumuiya ya Afrika Mashariki huku Kenya ikitwikwa mzigo wa kukisimamia na pia kutumwa katika maeneo hatari zaidi karibu na Goma ambako waasi wa M23 wakisaidiwa na Rwanda wamekuwa wakipigana na jeshi la DRC.

Afisa huyo ambaye aliomba tusimtaje jina alisema katika muhula wake wa mwisho ofisini, Uhuru alitumia diplomasia sana kuzungumza na Kagame na Tshisekedi, kuhusu umuhimu wa kikosi cha kudumisha amani na uthabiti.

Alijitahidi, pamoja na viongozi wengine wa EAC, kuhakikishia Kagame kuwa suala la usalama wa nchi yake litashughulikiwa akiacha kusaidia waasi wa M23, kuondoa wanajeshi wake DRC na kuruhusu kikosi cha EAC kutumwa huko. Kagame pia alikubali kuwa, kama taifa linalohusika katika mzozo huo, hangetoa wanajeshi kujiunga na kikosi hicho cha kanda, lakini atazingatia kulinda mpaka wa Rwanda.

Uhuru pia alisaidia kujumuishwa kwa DRC kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupanua jumuiya hiyo kutoka Bahari Hindi hadi Atlantic, ikiwa na watu zaidi ya 300 milioni na uwezo mkubwa wa kiuchumi.

Mbali na kujiunga na katika kupigania utajiri wa Congo, Kenya itanufaika na kwa amani. Bandari ya Mombasa ni lango muhimu la kupitishia bidhaa kutoka na kuelekea Mashariki ya DRC, Uganda, Sudan Kusini na Rwanda.

Kenya pia inatafuta biashara ndani ya Afrika, kuanzia ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama eneo muhimu la ukuaji wa uchumi. Kwa miaka mingi, Uganda imekuwa mshirika mkuu wa kibiashara wa Kenya, na watengenezaji bidhaa wa Kenya pia wanataka kupenya zaidi katika nchi zingine katika eneo hili.

Amani katika DRC itaongeza mara moja upatikanaji wa soko kubwa litakalopanuka kutoka eneo la mashariki hadi ndani ya nchi hiyo na pia kuimarisha njia za biashara kutoka Mombasa hadi ndani kabisa ya nchi hiyo tajiri kwa madini.

Kenya hailengi mali asili, lakini inaweza kuwa katika nafasi nzuri ya kutia nguvu nafasi yake kama kituo cha uchukuzi, mawasiliano na huduma katika ukanda huu.

Kulingana na afisa huyo wa Wizara ya Mashauri ya Kigeni, mikutano mitatu iliyoan-



Wanajeshi wa Uganda wakiwa karibu na mji wa Goli, eneo la Ituri, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, mnamo Mei 19, 2003.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Kikosi cha Hatua za Dharura cha Jeshi la Kenya (QRF) cha 01 Company, katika kambi ya kijeshi ya Embakasi mnamo Juni 15, 2021, kabla ya kutumwa kwa Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Kudumisha Amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (Monusco).
PICHA | FRANCIS NDERITU

daliwa na Uhuru jijini Nairobi ilinuiwa kuleta utulivu, nidhamu katika uchumi na uthabiti wa kijamii Mashariki ya DRC.

Kenya iliwekeza kwa kuleta makundi ya waasi kuhudhuria mkutano wa kwanza wa Nairobi ambako waasi hao walisema wako tayari kuacha mapigano iwapo serikali ya DRC itasikiliza matakwa yao.

Baada ya hapo, mapigano yalipungua katika eneo hilo, isipokuwa karibu na Boni, ambako M23 wanapatikana. Uhuru alikuwa kiongozi wa pekee aliyehudhuria kuapishwa kwa Rais Tshisekedi mnamo Januari 2019, alipomrithi Rais Joseph Kabila, ikiwa mara ya kwanza mabadiliko ya mamlaka kutokea kwa amani nchini DRC.

Kabila alikuwa ameingia mamlakani 2001 baada ya baba yake, Laurent Desire Kabila, kuuawa na mlinzi wake. Duru zinasema Uhuru na Tsishekedi walianza urafiki mara moja huku rais huyo wa DRC akitaka kuondoa nchi yake kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika Kusini (SADC) na kujenga uhusiano mpya na Afrika Mashariki.

Alikuwa pia akijaribu kuondoka katika "uhusiano wa kishughuli" ambao mtangulizi wake Kabila alikuwa amejenga na nchi yenye nguvu katika SADC, Jamhuri ya Afrika Kusini, ambayo juhudi zake za kijeshi katika nchi hiyo hazikuzaa matunda.

Juhudi za kimataifa chini ya Umoja wa Mataifa na nchi za Ulaya zenye nguvu pia hazikufanikiwa sana. Uhuru alitekeleza jukumu kubwa na kuonyesha ulimwengu kuwa Tshisekedi alikuwa kiongozi halali aliyehitaji kuleta uthabiti katika nchi yake yenye uwezo mkubwa.

Ni kutokana na juhudi hizo za mwanzo ambapo Mikutano ya Nairobi ilianzishwa. Mnamo Septemba, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianza juhudi zake za kwanza

DRC kuhamasisha serikali ya nchi hiyo kuhusu nguzo za kuunganisha EAC na mfumo wa utawala.

Mshirika mmoja muhimu katika mikutano hiyo alikuwa Katibu wa Wizara ya Mashauri ya Kigeni Kenya, Macharia Kamau, aliyehudhuria kama mjumbe maalumu wa Uhuru chini ya Mapngo wa Amani wa Nairobi. Alisema hali ya usalama katika mashariki ya DRC inaendelea kuzua wasiwasi mkubwa. "Tunapokaribisha Kikosi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mashariki ya

DRC, tunafaa kufanya hivyo kwa kutambua kuwa tishio linalotokana na makundi yenye silaha bado lipo na linahitaji ushirikiano wa karibu na washirika wetu wa kikanda na kimataifa kulikabili na kulikomesha," akaambia maafisa wakuu wa serikali ya DRC.

Alieleza kuwa Mpango wa Nairobi utaharakisha mbinu za kisiasa na kijeshi za kutafuta amani. "Kuna haja ya kila mtu kuongeza maradufu juhudi za kuendeleza mazungumzo na kutumia mbinu za kitaifa, kikanda na kimataifa za kutatua mizozo".

Alihakikishia ujumbe wa EAC na viongozi wa DRC kuwa serikali ya Rais

Ruto imejitolea kuendelea na kutia nguvu Mpango wa Nairobi. Mapema Juni, Uhuru aliandaa mkutano wa tatu wa Nairobi uliofuatwa na mkutano wa marais wa nchi wanachama wa EAC.

Marais kutoka nchi saba za wanachama wa EAC walifahamishwa kuhusu ripoti ya mkutano wa mkakati wa Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi ya nchi zote tano, na wakakubaliana kutoa wanajeshi kwa maeneo ambayo nchi zao zilitengewa na wakaidhinisha mkakati wa usalama wa wakuu wa majeshi. Kenya ilitwikwa jukumu la kusimamia operesheni yote, kutoa kamanda wa kikosi hicho cha kikanda huku majukumu mengine muhimu yakigawanywa kati ya nchi zingine.

Taarifa iliyotolewa baada ya mkutano wa Wakuu wa Nchi iliidhinisha ripoti ya kina ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Kenya Jenerali Robert Kibochi, mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Majeshi. Ripoti hiyo ilifafanua tatizo, ikaeleza uchanganuzi wa tishio, Muundo wa Operesheni (CONOPs), Hali ya Makubaliano ya Kijeshi (SOFA), Sheria za Ushiriki (ROE) na kanuni zingine za kisheria na kiufundi ili kuwezesha kuundwa kwa kikosi cha kikanda na vitengo vyake tofauti.

Viongozi wa Nchi waliagiza Kikosi cha Kanda kwa ushirikiano na vikosi vya kijeshi na utawala wa DRC kuleta uthabiti na kutafuta amani katika DRC na kushirikisha utekelezaji wa mpango wa kupokonya silaha makundi ya waasi.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Marais Tshisekedi, Museveni, Kagame, Salva Kiir wa Sudan Kusini na Evariste Ndayishimiye wa Burundi. Rais Samia Suluhu wa Tanzania aliwakilishwa na balozi wa nchi yake Kenya, John Steven Simbachawene. Marais hao waliagiza kusitishwa mara moja kwa mapigano pamoja na kuanzishwa kwa mpango wa kisiasa wa kuleta amani katika eneo hilo.

Mnamo Septemba, Tshisekedi alishuhudia kutiwa saini mkataba uliotoa idhini ya kutumwa kwa Kikosi cha Pamoja cha EAC. Katibu Mkuu wa EAC Peter Mathuki na Makamu Waziri Mkuu wa DRC, ambaye pia ni Waziri wa Mashauri ya Kigeni, Christophe Lutundula Apala Pen'Apala, walitia saini Mkataba wa Hali ya Kijeshi (SOFA) katika makao rasmi ya Rais jijini Kinshasa. "Mkataba huo unaruhusu kutumwa kwa Kikosi cha Pamoja cha EAC kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo na baada ya hapo, utathmini utafanywa," akasema Katibu Mkuu.

Makao Makuu ya kikosi hicho yalianzishwa na maafisa muhimu kuteuliwa wakiongozwa na Meja Jenerali Jeff Nyagah, Afisa wa Jeshi la Kenya anayeheshimiwa mwenye ujuzi mkubwa katika kikosi cha Kenya nchini Somalia.

Hata kabla ya kutia saini mkataba rasmi, Darubini ya Wiki imefahamu kuwa kutumwa kwa wanajeshi tayari kumeanza huku Kenya na Burundi zikiongoza katika maeneo zilizotengewa.


Maafisa wa kijeshi na Wizara ya Mashauri ya Kigeni Kenya walikataa kutaja idadi ya wanajeshi waliotumwa katika maeneo ya operesheni. Juhudi za kupata maelezo katika makao makuu ya EAC jijini Arusha hazikufaulu, lakini inasemekana kuwa, hata kabla ya jeshi la Kenya kutumwa kikamilifu, makundi madogo ya Kikosi Maalumu cha Jeshi tayari yamefika kuchunguza hali ilivyo.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ Wanakandarasi wa EPC China wanatawala ujenzi wa miundomsingi nchini



# SGR: MTEGO HATARI WA DENI

*Kuna wasiwasi kuhusu athari za mageuzi makubwa ya Rais katika bandari kwa uhusiano na benki inayokopesha Kenya pesa nyingi za miradi ya miundomsingi kwa wakati huu - The China Exim Bank*

● NA JAINDI KISERO

Matokeo ya hatua ya Rais William Ruto ya kuvunja ukiritimba ambao Reli ya Kisasa (SGR) imekuwa ikifurahia kuliko kampuni zingine za uchukuzi kusafirisha bidhaa hadi Nairobi yanapoanza kuonekana, maswali yameibuka kuhusu maana ya hatua hiyo kwa deni la Kenya la dola za Amerika 5 bilioni la SGR, na uwezo wa kifedha wa kudumisha mradi huo mkubwa zaidi wa miundomsingi kuwahi kutekelezwa Kenya kwa miongo kadhaa.

Jambo kubwa hata zaidi ni kuwa kuna wasiwasi kuhusu athari za mageuzi ya Rais katika bandari kwa uhusiano na benki inayokopesha Kenya pesa nyingi za miradi ya miundomsingi kwa wakati huu - The China Exim Bank.

Kulingana na sajili ya hivi punde ya deni la nje, deni ambalo Kenya ilidaiwa na China Exim Bank kufikia Juni 2021 lilikuwa Sh759.6 bilioni. Darubini ya Wiki imeona nakala ya mkataba wa 'Utoaji na Usafirishaji wa Mizigo hadi Depo la Kontena la Embakasi' ulioandikwa Septemba 30, na kutiwa saini na Mamlaka ya Bandari za Kenya na Shirika la Reli la Kenya, ambao lengo lake lilikuwa kuwajibisha KPA kuhakikisha kiwango fulani cha mizigo kati ya Mombasa na Nairobi kilisafirishwa kupitia SGR.

Mkataba unasema: "KPA itatumia KRC kama mchukuzi wa usafirishaji hadi Embakasi ICD - kwa mpango wa kuchukua au malipo-kiwango cha chini cha mizigo na mingine inayotajwa katika mkataba huu."

Mpango unaofahamika kama "mkataba wa chukua au lipa", ni makubaliano muhimu katika kandarasi ya mkopo wa SGR. Unajiri ukiwa na mpangilio wa wazi unaoeleza viwango vya utendaji, ikiwemo maelezo ya kina kama tani za chini kabisa za mizigo kuweza kulipia mkopo kwa siku, tani za chini kabisa za mizigo kuweza kulipia mkopo kwa mwaka, idadi ya magari moshi kwa siku na mizigo ya chini na muda wa kuisafirisha.

Ili kufunga serikali mikono hata zaidi, China Exim Bank pia ilihakikisha kuwa mkataba huo ulikuwa sehemu ya ahadi na dhamana ya kulipa mkopo. Unasema: "Ulipaji wa pesa zilizokopeshwa na ulipaji wa riba na ada za mkopo utadhaminiwa na, miongoni mwa zingine, mkataba wa huduma wa muda mrefu kwa lengo la kuhakikisha kiwango cha chini cha mizigo muda wote wa mikataba kitatozwa ada na kupokelewa na mhudumu wa mradi, ambazo zitatumiwa kudhamini ulipaji wa pesa zilizokopwa na riba."

Hivyo basi, kwa kupatia SGR ukiritimba wa kusafirisha mizigo hadi Nairobi, serikali ilikuwa tu ikitekeleza ilichotia saini katika mkataba wa mkopo na kufanywa kuwa dhamana kwa mkopo mkubwa na benki yenye ushawishi.

Bila kutoa onyo, Rais alitupa sehemu kubwa katika mkataba muhimu na benki yenye ushawishi katika pipa la taka. Haijulakini jinsi KPA itakavyobiliana na hali hii. Mkataba unaeleza kuwa, iwapo mizigo katika SGR itapungua chini ya kiwango kilichotajwa katika mkataba wa kuchukua au kulipa, ni lazima KPA itumie pesa zake kulipia upungufu huo. Ni wazi kabisa kuwa, makubaliano haya ni wajibu mkubwa kwa mamlaka ya bandari.

Lakini je, kuna uwezekano kwamba hali hii itamfanya Rais Ruto kubadilisha uamuzi wake? Kukiwa na kundi lenye ushawishi mkubwa la wamiliki wa malori barabarani na kwa kuzingatia kuongezeka kwa umaarufu wa wahudumu wa vituo vya makontena ya mizigo Mombasa, kubadilisha agizo hilo kunaweza kuwa vigumu kwa serikali mpya.

Swali ambalo wanaofuatilia kuhusika kwa China katika ufadhili wa miundomsingi Kenya watakuwa wakiuliza ni msimamo wa Rais Ruto kuhusu nguvu ambazo wanakandarasi wa EPC China wamekuwa nazo Kenya kwa miaka ishirini iliyopita. Kampuni ya China Roads and Bridges Company, iliyojadili mikopo ya SGR kwa niaba ya nchi - pengine ndiyo yenye ushawishi mkubwa miongoni mwa kampuni za kandarasi za China nchini Kenya.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

Serikali ya Rais Mwai Kibaki ilipoondoka, wanakandarasi wa EPC China waliokuwa wakitegemea serikali hiyo walijipata pabaya. Mfano mzuri ni masaibu yaliyokumba mradi wa mabilioni ya pesa wa Greenfield Airport, mradi wa Hazina Towers wa NSSF, mradi wa maji wa Mzima Springs, bomba jipya la mafuta kutoka Mombasa hadi Nairobi, mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Eldoret na mradi wa mawasiliano na ufuatiliaji wa Huduma ya Polisi.

Mbali na haya yanayojulikana, serikali mpya iliyoingia mamlakani ilishiriki vita vikali kurithi usaidizi wa wanakandarasi wa EPC China. Vita vya kuweka wanakandarasi wengine wa China walio na uhusiano wa kisiasa na watu wenye nguvu katika serikali iliyoondoka pia vimechacha.

Wakandarasi wa EPC China hutawala miundomsingi. Hii ndiyo sababu sajili ya deni la nje la Kenya leo imejaa madeni mengi ya China.

Katika miaka kumi iliyopita, nchi imekuwa ikitumia pesa kwa wingi, ikimwaga mamilioni ya dola za Amerika na Yuan za China - wakati mwingine mabilioni - katika kila ujenzi wa barabara, reli, bandari, laini za stima hadi kununua vifaa vya Shirika la Huduma la Vijana kwa Taifa, kuchimba visima vya nguvu za mvuke, kununua kamera za usalama hadi miradi ya ujenzi wa bwawa - mingi ambayo haijakamilika.

Wamekuwa wepesi wa kuunda na kutafuta inayoitwa mikopo iliyojadiliwa na wanakandarasi. Wakati huu, mwanakandarasi wa kawaida wa China ni mjanja anayezunguka mjini akiwa na jina la Kiingereza - Charlie, Lee, Tonny, Lily, Sandra, Johnny. Akiandamana na mshirika wa humu nchini – mara nyingi mtu aliye na ushawishi wa kisiasa na marafiki katika ofisi kubwa - raia huyo wa China atamwendea waziri au mkuu wa shirika la serikali akiwa na pendekezo la kutekeleza mradi mkubwa wa muundomsingi, akiwa na ahadi ya kupanga ufadhili wake. Wanakandarasi hao pia hukufanyia utafiti kuhusu manufaa ya mradi huo.

Katika awamu za mwanzo, Mkataba wa Maelewano hutiwa saini na waziri. Hii inafuatiwa na kutiwa saini kwa mkataba wa kibiashara na wizara au shirika la serikali. Hatimaye, Wizara ya Fedha itaalikwa kutia saini mkataba wa ufadhili na benki ya China, ambayo lazima itaingizwa kwenye shughuli hiyo na mwanakandarasi wa kigeni. Kwa njia hiyo, mkopo mpya ghali wa China utaingizwa kwa siri katika sajili ya deni la kitaifa.

Matajiri wa Kenya hupenda mipango ya aina hii kwa sababu kadhaa. Kwanza, inawezesha mtu kutia saini kandarasi za biashara ambazo hazieleweki vyema na Mikataba ya Maelewano kwa kukwepa taasisi za kupiga darubini kama Bunge, Mwelekezi wa Bajeti na Mhasibu Mkuu. Kwa njia hiyo, mtu anaunda njama na washirika wake wa kigeni kusukuma mradi katika mpango wa matumizi wa serikali bila kusubiri utengewe pesa na serikali.

Pili, mipango hiyo inaweza kuanzishwa na kukamilishwa bila kushirikisha miradi katika zabuni za kimataifa zenye ushindani kwa sababu inapangwa kama ya serikali na serikali nyingine.

Sababu ya tatu watawala wa siku hizi kupendelea wakandarasi wa EPC China ni kuwa ulipaji wa deni ndilo jukumu la kwanza la Hazina Kuu, kwa hivyo inalipwa hata kabla ya bajeti. Hivyo basi, ulipaji wa pesa zinazokopwa kutoka China huwa ni kama umehakikishwa.

Mnamo 2015, umma ulipata kuona mipango ya wakandarasi wa China inavyokuwa wakati aliyekuwa msaidizi wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Raila Odinga, Bw Herbert Ojwang, alipowasilisha bungeni kanda za mazungumzo kati yake na mwanakandarasi wa China ERPC, China Wuyi, ambayo alifichua maelezo ya mikataba aliyokuwa ametia saini na mwanakandarasi huyo.

Wanakandarasi wa China wataajiri ajenti wa humu nchini leo na kumtema kesho, kwa kutegemea upepo wa kisiasa unakovuma kuelekea Kenya. Kanda za Herbert Ojwang pia zilifichua kwamba, kuwa wakala au mlinzi wa kisiasa wa mwanakandarasi wa kutoka China kunaweza kuwa biashara kubwa Kenya.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



**Mkataba uliotiwa saini na Mamlaka ya Bandari za Kenya (KPA) na Shirika la Reli Kenya mnamo Septemba 30 unaitaka KPA ihakikishe kiwango fulani cha shehena kinasafirishwa kwa reli ya SGR kati ya Mombasa na Nairobi.** PICHA | KEVIN ODIT

# Ustawi wa viwanda bado ni ndoto kwa mataifa ya Afrika



• Na ALEX OWINO

Nchi nyingi za Afrika zinaeleza nia ya kustawi kiviwanda kama sehemu ya kauli mbiu za jumla kama "kustawisha viwanda Afrika". Hata hivyo, siamini viongozi wake na watawala wamejitolea au wana nia ya kujenga viwanda katika nchi zao zaidi ya kauli mbiu tupu kuwa "lengo" lao ni kujenga viwanda, hasa wakati wa uchaguzi.

Serikali ya Kibaki inatambuliwa kuwa bora zaidi na iliyoleta mabadiliko makubwa tangu uhuru. Aliingia mamlakani wakati ambao "mwanya wa kujenga viwanda" kwa kutumia muundo wa sera ya viwanda iliyokitwa kwa kuwa na wafanyakazi na uuzaji wa nje haukuwa umefungwa kabisa. Kama kuna serikali ambayo ilikuwa na nafasi ya kujenga viwanda Kenya, ilikuwa serikali ya Kibaki.

Lakini kufanya hivyo ilihitaji kuwa na sera ya viwanda. Hii inahusu kuchagua washindi kuunda mabingwa wa kitaifa (wa viwanda), kwa kupatia kipaumbele watengenezaji wanaoajiri watu wengi na kukumbatia ukuaji unaozingatia uuzaji bidhaa nje ya nchi. Baadhi ya hatua za ada na zisizokuwa za dada zilihitaji kuchukuliwa, sawa na sera ya mkopo iliyoelekezwa kufadhili mabingwa wa kitaifa kwa sababu ya viwango vya chini vya uwekaji akiba vya kitaifa. Sera kama hizo ziliwezesha mabingwa wa kitaifa wa viwanda nchini Korea Kusini ("Chaebols") na Japan ("Keiretsu") kufurahia mtaji bila matatizo katika miaka ya mwanzo zilipokuwa zikijenga viwanda. Lakini ole wao. Hakuna mojawapo ya hatua hizi ilitekelezwa!

Serikali ya Kibaki ilifuata mipango mizuri katika miaka ya mwanzo. Iliunda Mkakati wa Ufufuzi wa Uchumi kwa Uundaji wa Utajiri na Ajira mwezi Juni 2003 ambao wengi wanasema haukuwa tofauti na PRSP kutoka mashirika pacha ya kimataifa ya fedha. Ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la Kimataifa la Kwanza la Uwekezaji mnamo Machi 2004 na ikaanzisha Baraza la Kitaifa la Uchumi na Jamii (NESC) ili kuhakikisha serikali ilipata ushauri bora wa sera za uchumi. NESC iliendelea mbele kuunda Ruwaza ya 2030 kama Mwongozo wa Uchumi wa Kenya kwa

...Endelea Uk 11

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ MASUALA MUHIMU HUSHINDA MAHUSIANO YA KIKABILA

# MAFANIKIO MBALI NA NYUMBANI

*Mabadiliko katika mtindo wa kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu wa Agosti Agosti 9 yatokea katika viwango vya chini zaidi vya uwakilishi, ambako wanasiasa hutangamana na wapigakura*

• NA OSCAR OBONYO

Uteuzi wa Zacharia Mwangi Njeru kuwa Waziri wa Ardhi ni mojawapo ya habari njema kutoka kwa serikali mpya ya Rais William Ruto.

Njeru, aliyekuwa diwani mteule mbaye anatoka mtaa wa mabanda wa Bondeni, Nakuru, anaelekea kuwa mtu wa pili kutoka Kaunti ya Nakuru kuwa Waziri, baada ya shujaa wa uhuru Achieng'Oneko.

Wakazi wa Nakuru wanaposubiri kwa hamu kuona bendera ya waziri, ambayo ilipeperushwa eneo hilo mara ya mwisho mnamo 1966 na Oneko, aliyefungwa jela pamoja na Rais wa kwanza wa Kenya Jomo Kenyatta, hatua ya Ruto imerudisha kumbukumbu hiyo kuhusu mji huu ambao ni makao ya Wakenya kutoka sehemu zote nchini.

Mbali na Oneko, Mbunge wa kwanza wa Nakuru Mjini, aliyetoka Rarieda, Luo Nyanza, wakazi wa Nakuru pia walimchagua Lwali Oyondi kuwa Mbunge wao siasa za vyama vingi zilipoanza nchini mnamo 1992. Oyondi ni ndugu ya aliyekuwa Mbunge wa Butere, Martin Shikuku.

Tangu wakati huo, wanasiasa kadha kutoka nje ya Rift Valley wamechaguliwa wabunge katika Kaunti ya Nakuru, ishara kuwa siasa za ukabila si muhimu katika eneo hilo.

Maeneo mengine yameanza kuiga mtindo wa wakazi wa Nakuru kwa kuchagua wanasiasa wazaliwa wa maeneo mengine. Mfano wa hivi punde ni eneo bunge la Taveta, ambalo limemchagua John Bwire, katika uchaguzi mkuu wa Agosti 9.

Bwire ambaye asili yake ni Kaunti ya Busia, alimshinda mwanasiasa mkongwe na waziri wa zamani, Dkt Naomi Shabaan.

Inaaminika Bwire alinufaika kutokana na ushjndani wa kikabila kati ya Wataita na Wakamba ambao ni wengi katika eneobunge hilo. Huku wagombeaji wengi wa jamii hizo wakigawana kura zao, Bwire alitimiza msemo wa kiongozi wake wa chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka wa "kupitia katikati yao".

Hata hivyo, inasemekana Bwire aliendesha miradi manufaa kwa wakazi ikiwemo basari kwa wanafunzi, usambazaji maji katika hospitali na huduma za ambulanzi.

Isitoshe, Bwire ambaye ni wakili, amekuwa akitoa huduma za kisheria bila malipo kwa wakazi wanaokabiliwa na mizozo ya mashamba. Mbunge huyo, ambaye baba yake alizaliwa katika eneobunge la Funyula, Kaunti ya Busia, alizaliwa na kulelewa katika eneobunge la Taveta.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Demokrasia ya Vyama Vingi (CMD-Kenya), Frank Mukwanja, anasema mtindo huo wa wapiga kura kuchagua viongozi bila kuzingatia ukabila pia umedhihirika katika chaguzi za madiwani.

"Hatua ya wapiga kura kuchagua bila kuegemea ukabila na vyama pia imeonekana katika maeneo kadha nchini. Hii inaonyesha kuwa demokrasia nchini inaelekea kukomaa," anaeleza Mukwanja. "Wapiga kura walionyesha mfano mzuri kwa kukataa kupiga kura kwa kuzingatia mfumo wa suti uliokuwa ukipigiwa debe ya wagombea wakuu wa urais," akaongeza.

Kwa mfano, Simon Maina, diwani mpya wa Wadi ya Marachi Magharibi, eneobunge la Butula, Kaunti ya Busia, anaungama kuwa alichaguliwa kwa misingi ya sera, sio ukabila, katika uchaguzi mkuu uliopita.

Maina, mzaliwa wa Kaunti ya Nyandarua, anaongeza kuwa bidii na ushirikiano kati yake ndiyo mambo yaliyochangia ushindi wake.

Diwani huyo, ambaye anamiliki duka la jumla katika miji wa Bumala kando ya barabara ya Kisumu-Busia, anajihisi kuwa mwenyeji wa eneo hilo ambaye ana wajibu wa kutumikia jamii yake. Hiyo ni licha ya kuwa Maina, ambaye huzungumza Kiluo na Kiluhya kwa ufasaha, hutajwa kuwa "Wuod Okuyu" (mtoto wa Mkikuyu).

Diwani huyo huchangia maendeleo kama vile ujenzi wa makanisa na shule.

Janga la Covid



Mbunge wa Taveta John Bwire

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

-19 lilipotokea nchini mapema mwaka wa 2020, Maina alijitolea kusambaza misaada ya chakula kwa wakazi na taasisi mbalimbali eneo hilo, hatua ambayo iliwafanya wakazi kumpenda.

Mbali na Maina, aliyechaguliwa kwa chama cha MDG, kuna Peter Kipkoech Talam, aliyeshinda udiwani wa Wadi ya Bukhayo Magharibi, eneobunge la Matayos. Talam, ambaye anatoka jamii ya Kalenjin, ni afisa wa zamani wa Idara ya Magereza. Alishinda kiti hicho kwa chama cha ODM, kilicho wafuasi wengi katika Kaunti ya Busia.

Kilomita 107 kutoka Busia, tunampata Bw Charles Anyona Ogachi (mzaliwa wa Kisii), ambaye alishinda udiwani katika Wadi ya Mautuma, eneobunge la Lugari, Kaunti ya Kakamega. Ogachi aligombea kwa chama cha UDP kinachoongozwa na mbunge wa zamani wa eneo hilo, Cyrus Jirongo.

Mnamo 2017 diwani wa kwanza wa asili ya Luo Nyanza, Cyrus Omondi, alichaguliwa katika eneo la Kati ya Kenya. Omondi, kutoka Kaunti ya Siaya, alishangaza wengi aliposhinda udiwani wa Wadi ya Kahawa Wendani, eneobunge la Ruiru, Kaunti ya Kiambu.

Kwa misingi ya tafiti za awali za CMD, Mukwanja anasema wakazi wa maeneo ya mashambani huzingatia ukweli wanapopiga kura. Wanazingatia zaidi mahitaji yao ya kimsingi kuliko vyama au miungano ya kisiasa.

Hii ndiyo maana "mgeni" anayejitokeza na kuonyesha anajali masilahi ya wakazi hungwa mkono katika uchaguzi.

Hali ni tofauti katika maeneobunge ya mijini ambako ukabila na miegemeo ya kisiasa ya wagombeaji ndiyo mambo yanayopewa uzito na wapigakura. Katika maeneo hayo wanasiasa hushawishi wakazi kutoka makabila yao kujiandikisha kuwa wapigakura katika maeneobunge fulani kwa lengo la kushinda wapinzani wao.

Mchezo huu wa kisiasa ndio umetumitiwa na wanasiasa wa Nairobi, wakiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, mawaziri wa zamani Fred Gumo na Maina Kamanda, tangu miaka ya 1990s.

Na hii ndiyo maana baadhi ya maeneobunge kama vile Kibra, Langata, Westlands na Starehe, kwa miaka mingi imewakilishwa na wabunge kutoka makabila fulani.

Lakini hali ni tofauti katika eneobunge la Kisumu Mjini Mashariki ambalo limewakilishwa kwa mihula minne mfululizo na Mbunge Shakeel Shabbir, mwenye asili ya Kihindi. Shabbir ni miongoni mwa wabunge wa Luo Nyanza ambao wamehudumu kwa kipindi kirefu. Amehudumu kwa mihula minne sawa na mwenyekiti wa ODM John Mbadi na Mbunge wa Suba Kaskazini Millie Odhiambo isipokuwa hawa wawili waliteuliwa kwa kipindi kimoja kila mmoja.

Sawa na Bwire (mbunge wa Taveta) Shabbir anapendwa na wakazi kutokana na kujitolea kwake kushughulikia changamoto zinazokumba wakazi.

Isipokuwa 2007 na 2013, alipochaguliwa kwa chama cha ODM, Shabbir amechaguliwa mara mbili akiwa mgombeaji huru na kushinda wimbi kali la chama hicho cha Raila.

Hali kwamba si Mluo inamruhusu kuhudumia wakazi bila kuwabagua kwa misingi ya kikoo. Kama anavyosema, kuwa mgombeaji huru, humweka huru kutokana na vyama na viongozi wake. "Nilizaliwa Kisumu na nitakufa na kuzikwa hapo. Kimsingi mimi ni Mluo, shida ni rangi ya ngozi yangu," anasema Shabbir, ambaye huzungumza Kiluo kwa ufasaha.

Bw Rahim Dawood na Bw Swarup Mishra, ambao pia ni wa asili ya Kihindi, pia walipata matokeo tofauti Agosti huku Dawood akihifadhi kiti cha Imenti Kaskazini kwa mara ya tatu naye Mishra akipoteza kiti chake cha Kesses kutokana na wimbi la UDA.

Kwa upande mwingine, Junet Mohamed, Mbunge wa Suna Mashariki, alirudi Bunge kwa muhula wa tatu. Lakini tofauti na Shabbir, mwanasiasa huyo wa asili ya Kisomali, bado ni mwanachama wa ODM.

Bw Mukwanja anasema mtindo wa wapigakura kufanya uamauzi bila kuzingatia ukabila na vyama vya kisiasa ni ishara kuwa wameamua kusimamia hatima yao ya kisiasa.

Anasema hali hiyo ambayo inashuhudiwa hasa katika ngazi ya wadi, inaonyesha kuwa wapigakura wamechoka kuwa mateka wa vyama na wakuu wa vyama hivyo.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Ustawishaji wa viwanda ni muhimu kwa nchi za Afrika

...Kutoka Uk 9

muda mrefu. Maeneo ya EPZ kama ya kwanza ya sera ya uuzaji nje wa viwanda, na Maeneo Spesheli ya Uchumi (SEZ) yametumiwa na nchi zinazoendelea kama vifaa muhimu vya kujumuisha viwanda katika uchumi wake.

Mnamo Juni 2004, nilitayarisha utafiti wa kwanza wa EPZ kuwahi kufanywa Kenya (kupitia jarida la ujasusi wa masoko) kwa mchango kutoka kwa Shirika la EPZ na Wizara ya Biashara na Viwanda. Mojawapo ya matokeo muhimu kutokana na utafiti huo ilikuwa maeneo ya kwanza ya EPZ Kenya yalianzishwa kama miradi ya maendeleo bila kuambatanishwa na mifumo ya uongezaji thamani ya humu nchini.

Karibu muongo mmoja nikiwa mshauri wa Mradi wa Wizara ya Fedha (FLSTAP), nilipendekeza Sera ya Viwanda na kusaidia kuunda sera ya SEZ Kenya na rasimu ya Mswada wa SEZ 2012. Zote tatu zilikubaliwa na kusitishwa hadi 2015 wakati sheria hafifu ya SEZ iliundwa kama pingamizi ya Wizara ya Fedha kutoza ushuru vitu vilivyopeanwa bure na vya kutia motisha.

Shirika la SEZ lililoanzishwa chini ya sheria ya SEZ ya 2015 halijawahi kutekelezwa kikamilifu miaka 7 baada ya kuanzishwa na karibu muongo mmoja baada ya mimi kuunda sera "halisi" ya SEZ na Mswada wa 2012!

Hali hiyo ilikumba Mpango Mkuu wa Ustawi wa Utafiti wa Viwanda Kenya (MAPSKID) ambao shirika la JICA la Japan liliunda kwa Kenya mnamo 2007. Ulitupwa kwa haraka katika "makaburi" ya sera za kitaifa za Kenya katika bustani ya ndoto zilizotibuka za kuleta "ustawi wa viwanda Kenya".

## Kutambua nia ya kujenga viwanda

Ruwaza ya 2030 inaeleza wazi "nia" ya kustawisha viwanda Kenya. Ileweka malengo ya kuanzisha "sekta kubwa, ya aina mbalimbali na yenye ushindani" ambayo inakua kwa asilimia 10 kwa mwaka na kuchangia asilimia 15 ya pato la nchi (GDP). Ilitambua viwanda kama sekta muhimu ya uchumi na kuanzishwa kwa maeneo mawili spesheli ya uchumi na bustani tano za viwanda vidogo kama miradi mikuu. Hakuna lililotekelezwa kati ya haya. Wakati huo huo, mchango wa viwanda katika GDP Kenya unaendelea kushuka kutoka asilimia 12.5 hadi asilimia 7.5. Nia ya Ruwaza ya 2030 ya kustawisha viwanda Kenya ilikufa kabla ya haijazaliwa!

## Ukweli wa kupungua kwa viwanda

Naona tofauti ndogo katika umma Kenya kuhusu nia ya kukubaliana kustawisha viwanda. Viongozi wengi wanakubaliana kwa mapana kuhusu na hata jinsi ya kuutekeleza - kwa mfano kwa kuanzisha Maeneo Spesheli ya Uchumi.

Kenya inafaa kuweka uwezo mkuu na uwezeshaji ili kuwa na utendaji katika taasisi hizo kuu ikiwa kweli inataka kufanikisha nia yake ya kustawi kiviwanda. Haitoshi kutangaza "nia" ya kustawi kiviwanda huku ikikosa kufanya juhudi za kujenga uwezo au uwezeshaji wa kutekeleza sera ya viwanda.

Serikali inayokuja inarithi nchi inayoelekea kinyume na "kupungua kwa viwanda" haraka hata kabla ya kustawi "kiviwanda". Mwongozo wake wa muda mrefu wa uchumi (ruwaza ya 2030) na mipango yake mikuu ya viwanda kama MAPSKID imesahaulika.

Wakenya wanatazama tu nchi "zilizochelewa" kama Malaysia (kutoka 1978) na Vietnam (kutoka 1994) zikikumbatia sera za viwanda na kuanza ustawi wa viwanda kwa kasi na kusonga kutoka nchi zinazoendelea hadi zilizoendelea.

***Bw Owino ni mshauri na mtaalamu wa sekta ya fedha***

*-Imetafsiriwa Na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong Un, akizuru chuo cha mafunzo ya ulengaji shabaha cha Mangyongdae Revolutionary Academy, eneo la Pyongyang, kutazama wanachuo wakifyatua bastola. PICHA I AFP



Mtunzaji wa Ndovu Kiapi Lakupanai akicheza na ndama wawili katika Kituo cha Kutunza Ndovu cha Reteti, Mbuga ya Wanyama ya Namunyak, Samburu, mnamo Oktoba 12. Kituo cha Kutunza Ndovu cha Reteti kimelemewa na shughuli za uokoaji na ndama wengi mayatima na wengine waliotelekezwa na mama zao kutokana na ukame wa sasa. PICHA I MAKTABA



Rais wa China Xi Jinping, akiwasili kwa sherehe ya kufunguliwa kwa Kongamano la 20 la Chama cha Kikomunisti cha China, katika ukumbi wa Great Hall of the People, jijini Beijing, mnamo Oktoba 16. PICHA I AFP




Mwanandondi wa Amerika Deontay Wilder (kushoto) amwangusha mwanandondi Robert Helenius wa Sweden Robert Helenius katika raundi ya kwanza ya pigano lao la raundi 12 la WBC uzani wa juu katika ukumbi wa Barclays Centre, Brooklyn, New York, mnamo Oktoba 15. PICHA I MAKTABA



Farasi aruka juu akitayarishwa pamoja na wengine na waendeshaji farasi wa Lesotho kabla ya kuanza kwa mashindano ya kitamaduni ya mbio za farasi katika mji mdogo wa Semonkong, ulio karibu na milima ya Maluti, mnamo Oktoba 15. PICHA I AFP




Wahudumu wa afya wabeba jeneza wakati wa mazishi ya pamoja ya waandamanaji 27 na maafisa sita wa polisi katika eneo la makaburi la Bolima, Wilaya ya Waterloo, mjini Freetown, Sierra Leone, mnamo Oktoba 17. Waliuawa wakati wa ghasia za Agosti. PICHA I AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La

# Vijana



# GUMZO PESA

*Ingawa utayarishaji wa podcast ni biashara mpya Afrika, Eli Mwendwa ameitumia kupata umaarufu na kuunda pesa kupitia mazungumzo ya mtandaoni kuhusu mambo yanayokabili wanaume lakini hawayazungumzii*

NAFASI YA VIJANA

# UKIMWI: SI MAAFA TU

**MAZURI:** Licha ya hofu iliyosababishwa na maambukizi haya, yalileta mabadiliko mengi makuu katika taaluma ya matibabu

• NA MOSES OJUANG'

'Vuta mema hata kutoka kwa ibilisi…' Ni uchungu unaosababisha fikra kuwaza; hali ya furaha iliyotulia bila kuvurugwa ingefanya kutafakari, kusaili na uvumbuzi kutokuwa na maana.

Wakati fulani miaka ya 1980, jirani mzee aliyekuwa mkorofi aliniuliza nilizaliwa mwaka gani; nilimwambia upesi na akaangua kicheko. Aliniam mwaka huo alikuwa anatibiwa maambukizi yake ya tatu ya kisonono.

Ni lazima alikuwa amehitimu umri wa kuwa baba yangu maadamu tayari alikuwa ameanza kushiriki mapenzi nilipokuwa nikizaliwa. Hizo zilikuwa enzi za kushiriki ngono bila malipo. Kila Jumatatu, hospitali zilikuwa zinajaa wagonjwa wa Maradhi ya Zinaa (STDs). Wangepiga foleni mbele ya wauguzi wajeuri waliokuwa wakichemsha sindano butu tayari kuzisukumiza kwenye makalio yao; kabla ya kudungwa sindano hiyo yenye uchungu, ilikuwa sharti wanywe pakiti ya maziwa hapo mbele ya mwuguzi. Kila mtu alijua walichokuwa wakitibiwa.



Yote haya yalitendeka kabla ya kufika kwa Ukimwi. Ilikuwa enzi ya kutojali ambapo watu walijua kitu kibaya zaidi ambacho kingetokana na kula uroda ni mtoto au kisonono. Ugonjwa huo ulikuwa na tiba na walioambukizwa walichukulia masaibu yao kuwa nembo ya heshima; Ungepongezwa na wenzako kwa kuwa 'mwanamume'.

Kisha HIV ikafika kwa kishindo na kitumbua kikaingia mchanga. Mambukizi ya Ukimwi yalisambaa kama moto nyikani. Walioambukizwa kwa namna fulani hawakujua hali yao, hivyo waliendelea kueneza virusi hivyo bila kujua.

Kufikia mwanzo wa 1990, waliopata Ukimwi walianza kufa vifo vya kutisha sana. Foleni katika kliniki za kutibu kisonono zilipungua na taaluma ya matibabu ikalazimika kufanya mageuzi katika mifumo ya tiba. Vifaa vyenye umbo la kibofu vilivyokuwa vikitumiwa kuchemshia sindano vilisukumwa kando; Hapakukuwa tena na kutumia sindano kwa watu zaidi ya mmoja.

Mambo waliyokuwa wakifanya kwa kutumia mikono yao ni sharti yangefanywa wakiwa wamevaa glavu. Shughuli ya kutoa damu iliyofanywa awali bila umakinifu sasa ilikuwa chukizo: ni sharti damu ingepimwa kabla ya kukubalika kwenye hifadhi ya damu. Hata watu waliokuwa wakijitolea kutoa damu walipungua kwa sababu walihofia kupimwa Ukimwi kabla ya kutoa damu.

Licha ya wingu la hofu kutokana na virusi hivyo, kuna mengi ambayo walio hai wanafurahia leo hii. Ni sharti mambo yangebadilika kwa dharura ili kudhibiti maambukizi mapya. Sindano butu zilitoweka, nyembe zilizotumiwa kwa wagonjwa wengine zilisahaulika, uzoaji na kuharibu takataka za kimatibabu ukageuka mchakato unaofanywa kwa umakinifu zaidi. Yote haya yalitokana na HIV na Ukimwi.

Kwenye ulingo wa jamii, marekebisho machungu yalilazimika kufanywa. Itikadi zilizopitwa na wakati kama kurithi wake, tamaduni zilizojikita mizizi miongoni mwa waliozifuata, zilitikiswa kabisa.

Wang'ang'anizi sugu waliokataa mabadiliko waligeuka mafunzo ya kutisha kwa waliodiriki kukabili virusi hivyo. Ilikuwa ubatizo wa moto na kifo uliosomba polepole itikadi zilizopitwa na wakati. Enzi mpya ilichukua usukani.

Viongozi wa kidini waliojichukulia kuwa watakatifu zaidi na waliofikiri virusi hivyo viliwaathiri watenda dhambi pekee walipigwa na butwaa vilipovamia washirika wao. Virusi hivyo vilikuwa vimepenya zaidi katika familia na kuvamia hata watu wakaidi waliokuwa wakiteketeza kondomu hadharani ili kutangaza upangaji uzazi kama upotovu wa kimaadili.

Dini, sayansi, utamaduni na serikali ziliungana kupambana na Ukimwi. Sauti hii ya pamoja haikuwa imewahi kusikika hapo mbeleni kuhusu suala moja. Ufanisi ambao nchi yetu ilipata kutokana na ugonjwa huo ni wa ajabu.

*Bw Ojuang'ni mchanganuzi wa masuala ya kijamii*

*Je, wewe ni kijana mwenye maono? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni na mtazamo wako kuhusu masuala ibuka kupitia:* ***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

## WANAVYOSEMA



**Ayub Yensis Adan**

Kuvunjiliwa mbali kwa kikosi maalumu cha Idara ya Uchunguzi wa Jinai kutokana na madai kuwa maafisa wake walijihusisha na mauaji ya kiholela si hatua ya kushangaza. Natumai visa vya mauaji na kukamatwa kwa watu kiholela vilivyotekelezwa na maafisa w kikosi hicho vitachunguzwa na watakaopatikana na hatia ya kutumia vibaya mamlaka yao washtakiwe. Kenya inahitaji maafisa wa usalama wanaozingatia utaalamu.

*— Mwanafunzi, Chuo Kikuu cha Daystar*



**Albert Maloba**

Rais William Ruto anafahamu anachofanya kwa kuvunjilia mbali kitengo spesheli cha DCI, ikizingatiwa kuwa alihudumu kama wa pili kwa mamlaka kwa kipindi cha mwongo mmoja uliopita. Hapo awali ameshutumu idara ya polisi kwa ukatili na kukosa kuzingatia utaalamu, hivyo basi ni wajibu wake kusafisha kikosi hicho na kuhakikisha Kenya na Wakenya wanalindwa dhidi ya vitisho kutoka humu nchini na nje.

*— Kiongozi wa Baraza la Vyuo Vikuu Kenya*



**Cynthia Tanui**

Ukosefu wa usalama si jambo geni Kenya. Kila uchao tunasikia visa vya watu waliotoweka, huku baadhi wakipatikana wakiwa wamekufa. Ni wajibu wa Idara ya Polisi kuhakikisha Wakenya wako salama. Rais William Ruto ana jukumu la kuhakikisha Wakenya wana imani katika vikosi vya usalama na kutetea haki kwa familia za wahasiriwa wa ukatili wa polisi.

*— Mahusiano ya Wateja*



**Raisy Rono**

Ninapongeza amri ya Rais ya kuvunjilia mbali kikosi maalumu cha DCI. Si vyema kuwa na watu wanaotarajiwa kuimarisha usalama kugeuka watekelezaji wa ukatili na kiini cha machungu nchini. Naamini hilo ni suluhisho la muda mfupi na ninatumai Rais na timu yake watazindua mpango madhubuti.

*— Mwanafunzi*

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU



NA WAGA ODONGO

# BANGI IFANYWE HALALI KENYA

**Dawa:** Bangi imehalalishwa kabisa au kwa kiasi fulani katika mataifa ya Netherlands, Australia, Canada, Chile, Colombia, Costa Rica, Portugal, Afrika Kusini, Uhispania na Uruguay



Niliangalia takwimu za mwaka jana kuhusu uhalifu hasa nikiangazia kwa makini kitengo cha mihadarati. Ripoti hiyo, inayopatikana kwenye tovuti ya Polisi Kenya, inaonyesha Kenya haina tatizo "hatari la dawa za kulevya", ina tatizo la bangi. Katika karibu robo tatu ya kaunti zote nchini mihadarati pekee ambayo polisi wamenasa ni bangi. Visa vya kuwakamata watu kuhusu bangi na kugunduliwa kwa bangi pia vilikuwa vingi huku kila kaunti ikiwa na angalau kisa kimoja. Rekodi hiyo pia inaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 95 ya visa vyote hatari vya mihadarati vinatokana na bangi.

Kwa kuzingatia bangi, utekelezaji wa sera kuhusu mihadarati haujafua dafu. Kama tungeweka sera kali inayopiga marufuku kabisa ambayo ingeamuru kukamatwa kwa kila mtu ambaye amewahi kuwa na bangi, basi taasisi zetu za elimu ya juu zingebaki tupu na idadi ya washukiwa ingefilisisha Huduma ya Magereza.

Bangi ni maarufu sana kiasi kwamba kuna makundi mengi kwenye mtandao wa kijamii wa Facebook yanayowaunganisha wauzaji na wanunuzi kulingana na eneo. Kwa walio wasiri, mtandao wa kijamii wa Snapchat ulio na mfumo unaowezesha kutengea jumbe wakati na kuzuia usambazaji wa jumbe, sio afueni tu kwa usambazaji wa picha za kuibua ashiki, ni kipenzi kwa walanguzi wa mihadarati wanaoweza kutangaza bidhaa zao huku wakiifanya vigumu kufuatiliwa mitandaoni. Ninaweza kukisia kuwa zaidi ya nusu ya watu wazima walio chini ya umri wa miaka 35 hawafikirii bangi inafaa kuchukuliwa kama mihadarati hatari.

Ikizingatiwa kuwa bangi imesambaa sana na wateja wake kuongezeka, tunaagiza maafisa wa polisi kutekeleza sheria ambayo imepoteza kibali cha umma. Mpango wa kuhalalisha bangi kote duniani umejikokota, lakini majira yanabadilika na itakuwa upumbavu kwa Kenya kupuuza mkondo huu mpya.

Kwa hesabu yangu, bangi imehalalishwa kabisa au kwa kiwango fulani katika nchi za Netherlands, Australia, Canada, Chile, Colombia, Costa Rica, Portugal, Afrika Kusini, Uhispania na Uruguay.

Bangi ina matumizi fulani ya kimatibabu. Tuna kliniki mbili katika miji miwili nchini zinazotumika kusaidia walio na uraibu wa matumizi ya heroni, ambayo ni mihadarati hatari zaidi. Kliniki hizo mbili zinatambuliwa ulimwenguni kote kwa kazi yake ilhali kuhusu bangi, mihadarati inayopatikana zaidi na ambayo ikilinganishwa na heroni, ni salama zaidi, Kenya imekuwa ikijikokota.

Bangi kwa sasa imeorodheshwa kama dawa ya kulevya chini ya Kifungu cha Sheria Nambari 4 cha 1994 kuhusu Dawa za Kulevya na Mihadarati na faini zinazotozwa zinaweza kufikia mara tatu ya thamani ya mihadarati iliyonaswa. Mapema mwaka huu tuliona vichwa vya habari kuhusu walanguzi waliohukumiwa vifungo vya miaka 50 kwa kuuza kile ambacho katika baadhi ya mataifa ni sawa na viwango vilivyowekwa na serikali.

Mamlaka ya Kitaifa kuhusu Kampeni Dhidi ya Pombe na Dawa za Kulevya (Nacada) nayo imekuwa kizingiti zaidi badala ya msaidizi kuhusu mihadarati. Ingali inataka adhabu zilizopo kuhusu kosa la kupatikana na mihadarati ziimarishwe badala ya kutafuta namna ya kuhalalisha bangi.

Nacada imeshikwa mateka na waumini sugu wenye itikadi kali za kidini. Bosi mmoja aliyeongoza shirika hilo zamani alidai kwa kiburi kuwa bangi itahalalishwa Kenya "akiwa maiti." Inasikitisha kiongozi wa taasisi iliyotwikwa jukumu la kutoa ushauri kuhusu mihadarati anapotangaza kwa majivuno hadharani kuwa hawezi kutikiswa na ushahidi wa kisayansi. Bodi ya Nacada kwa sasa ina wanachama ambao ujuzi wao pekee wa kimsingi unategemea misingi ya kidini, jambo ambalo nafikiri halifai.

Madhehebu ya kidini hupagawa na sarakasi kila mara upepo wa bangi unapoelekea upande wao. Wao ndio kikwazo kikuu kwa mageuzi yoyote yanayojikita kwenye ushahidi.

Jinamizi la matumizi ya bangi linatokana na kuwa serikali haifanyii majaribio na kudhibiti mihadarati hiyo, sawia na pombe na tumbaku. Uraibu wa dawa za kulevya ni suala la kimatibabu na kijamii, hivyo basi umaarufu wa bangi daima utabakia kutoathiriwa na urefu wa vifungo vya jela au marufuku za serikali.

Huenda usifanikiwe kutekeleza hali ya kutotumia mihadarati kupitia sheria. Matumizi ya mihadarati yanakabiliwa na unyanyapaa kwa namna ambayo kunenepa kupita kiasi hakuangaziwi ingawa hali hizo mbili zina uhusiano. Kuwa na uraibu wa kutumia heroni hakupaswi kuwa hatia zaidi kushinda uraibu wa kubugia pombe au kula kupita kiasi.

Athari zozote kutokana na dawa za kulevya ni bora zishughulikiwe kupitia sheria badala ya kuwaacha vijana mikononi mwa michafuko na maslahi ya kibinafsi ya soko ambapo inaweza kuvurugwa kwa kuongezwa chembe hatari.

Ni rahisi kufafanua kuwepo kwa chembe za bangi ambazo zimehusishwa na matatizo ya kiakili. Tuna mfumo ambao bangi inayoundwa haifanyiwi majaribio, haidhibitiwi na haitozwi ushuru, ambao ndio chanzo cha matatizo yote haya.

Funzo kutokana na historia ni kuwa marufuku husababisha aina nyingine za mihadarati yenye nguvu zaidi. Wakati wa marufuku ya pombe Amerika katika miaka ya 1920, watu walianza kubugia dawa inayotumiwa kuhifadhi viumbe, maarufu kama formalin, badala ya pombe. Ni sharti kwa namna fulani bangi isambazwe chini ya udhibiti wa serikali ili tutahakikishe usalama wake.

Pombe ni mihadarati yenye nguvu zaidi na ina athari sugu zaidi kijamii kushinda bangi. Nenda katika mji mdogo Ijumaa usiku ujionee gharama ya pombe katika jamii. Utapata vita, kutapika, kukojoa katika sehemu za umma na uchokozi kwa wengine bila sababu.

Je, mtu anaweza kuchagua mtoto mlevi wa pombe mvutaji bangi? Hata ni kama mzaha kuuliza swali hilo kwa sauti. Hatuna budi kuwa na mjadala wa watu wazima sio tu kuhusu bangi, bali mihadarati yote, kwa kuzingatia sayansi na kupunguza madhara.

Bw Odongo ni mhandisi wa Datakanzi

*wagaodongo@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SHUGHULI TOFAUTI

# MTU WA VIPAWA VINGI

**KAZI CHUNGU NZIMA:** Pavraj ni mtaalamu wa kuchanganya vinywaji, mtaalamu wa masuala ya tekinolojia na mpishi hodari

• NA EDDY ASHIOYA

Ninakutana na Pavraj Singh akifurahia mkate aina ya burger katika mkahawa wa The Oval, mtaa wa Westlands na anakunja uso ninavyofanya usiku ninaposoma kazi za waaandishi wengine na kufikiria: "Hii ni nzuri; hebu niweze kuiiga."

Miongoni mwa kazi nyingi anazofanya Pavraj ni utaalamu wa kuchanganya mvinyo, mtaalamu wa tekinolojia na mpishi hodari. Pia, ana ile sura nzuri ambayo tovuti za uvumi Nairobi zinaweza kufurahia kuandika kichwa cha habari kama : "Kutana na mchanganyaji vinywaji wa Nairobi anayekosesha wanawake wa Kenya usingizi."

Tumekutana ArtCaffe kwa mahojiano, mojawapo ya mikahawa inayotembelewa na watu wa kila aina na bado inaweza kudumisha upekee wake. Tatizo langu tu ni muziki wa aina ya Muzak unaotoka kwa vipaza sauti. "Mimi ni mtu wa talanta nyingi," anaanza Pavraj," mimi nimesomea upishi lakini napenda sana kuchanganya mvinyo. Lakini nimekuwa katika sekta ya tekinolojia maisha yangu yote," anasema, akisindikiza maneno hayo na pombe. Anayosema ni maisha yake yote, ni miaka 27.

"Nilitolewa katika kampuni ya Tekinolojia ya Kifedha, nikaja Nairobi kutoka Canada. Kazi yangu ya kwanza ilikuwa kuhudumia wateja na kutoka hapo nilipanda cheo hadi kilele." Alijipata akifanya mambo mawili yanayokinzana - kuwa mtaalamu wa tekinolojia ya fedha mchana na kuchanganya mvinyo usiku. Na usingizi je? Usingizi kwake ni kwa waliokufa.

"Nilianza kuchanganya mvinyo kama mzaha. Nilikuwa nikuhudhuria hafla nyingi za kutangaza bidhaa na kila Jumatano, walikuwa na tabia ya kwenda baa huko Tapas. Wamiliki wake walinialika kuwahudumia, kitu ambacho nilifanya mara moja kwa wiki, kisha ikawa mara mbili na taratibu ikawa kitu ninachopenda."

Fintech, anasema, ndiyo taaluma yake. Fintech ni ufupi wa "tekinolojia ya fedha", inayomaanisha kampuni zinazotumia tekinolojia kushindana na mbinu za kawaida za ku-

**Ufadhili wa bidhaa sio kitu kipya Kenya. Kinyume nao, katika ufadhili wa bidhaa, kampuni, na hapa tunazungumzia Aspira, inafadhili bidhaa kwa niaba yako na unawalipa kwa awamu kila mwezi. Haina hatari yoyote kwa mnunuzi na unapata bidhaa yako - ni kama kukopa kutoka kwa mtu ili kulipa mwingine. Ushindi mtupu.**



Pavraj Singh ni mtaalamu wa masuala ya pesa, mpishi na mchanganyaji vinywaji.
PICHA | JEFF ANGOTE

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

**Nilianza kuchanganya mvinyo kama mzaha. Nilikuwa nikuhudhuria hafla nyingi za matangazo na kila Jumatano walikuwa na tabia ya kwenda baa huko Tapas. Wamiliki wake walinialika kuwahudumia, kitu ambacho nilifanya mara moja kwa wiki, kisha ikawa mara mbili na taratibu ikawa kitu ninachopenda**

Pavraj Singh

toa huduma za kifedha. Mfano ni blockchains, Cloud Computing na Big Data.

"Sisi sio kama benki. Tunafadhili bidhaa, ambazo ni mikopo isiyo na dhamana au uwekezaji mkubwa ulio na faida kubwa. Huwa tunafadhili moja kati ya maombi kumi, na kuifanya kuwa kali sana na yenye ulinzi. Tunaifanya kuwa rahisi kwa mikopo isiyohitaji udhamini."

Hii inanikumbusha kuwa Wakenya walikopa Sh1.6 bilioni kwa siku kupitia mikopo ya Fuliza katika mwaka mmoja uliopita. Sisi ni nchi inayopenda madeni sana.

"Huo ni ukweli lakini huwa tunachunguza walioorodheshwa kwa kutolipa mikopo. Sote tuko na kiwango cha madeni, uwe umechukua mkopo au la. Hatupatii mikopo walio katika hatari kubwa ya kutolipa," anasema Pavraj.

"Unaona, katika kampuni ya Aspira, tunawezesha Wakenya kwa kuwapa ufahamu mkubwa kuhusu masuala ya fedha. Tunapopata mteja ni juu yake kuchagua, na hivyo basi kujenga historia yake ya mikopo." Lakini sio kila mtu ana simu za kisasa, na ndiyo sababu wana mabalozi wa chapa yao na maajenti wa nyanjani wanaosajili wateja kwa mikono.

Ufadhili wa bidhaa sio kitu kipya Kenya. Kinyume, katika ufadhili wa bidhaa, kampuni, na hapa tunazungumzia Aspira, inafadhili bidhaa kwa niaba yako na unawalipa kwa awamu kila mwezi. Haina hatari yoyote kwa mnunuzi na unapata bidhaa yako - ni kama kukopa kutoka kwa mtu ili kulipa mwingine. Ushindi mtupu.

Je, Fintech imemfunza nini kuhusu tabia za kifedha za Wakenya? "Inaleta uraibu lakini kwa sababu nzuri tu. Biashara zikianza huwa hazina pesa. Sio rahisi kupata pesa." Anasema hofu kubwa kuhusu pesa ni wakati akaunti yake ya benki haina pesa na hajui zilikoenda. Lakini kufikia sasa, mambo ni mazuri. Anataja kufaulu kazini kuwa kutumia pesa vizuri. "Kama naweza kuwekeza katika kitu kinacholeta pesa zaidi siku zijazo, kwa nini nisifanye hivyo?

Pavraj anajionyesha kuwa mtu ambaye kwake pesa ni muhimu sana. Anazungumza pesa, kupumua pesa na kuishi pesa. Je, ni kitu gani cha kwanza anachoweza kuambia watu walio na pesa ambao hawajui wazifanyie nini?

"Ningewaambia waziweke kwa Sacco. Au waziweke kwenye akaunti ya amana ya kudumu ikiwa benki inatoa viwango vizuri. Kama hauhitaji pesa hizo, zihifadhi. Napenda kuchanganya mvinyo na ninajua ninakotaka kuwekeza."

"Unavyotafuta pesa sana, zitakuhepa zaidi. Nambia watu wafanye kazi kwa akili, sio kwa bidii. Kama haufanyi bajeti, basi utajiumiza. Wekeza kwa kitu ambacho kitakupatia faida."

Warren Buffet angefurahi kwa hili. Au ni Aliko Dangote? Kuhusu watu kama hao, ni nani amekuhimiza zaidi katika safari yako na pesa? "Mimi mwenyewe. Nimekuwa nikifanya kazi kwa miaka tisa sasa. Nilianza kufanya kazi katika Fintech nikiwa na umri wa miaka 19. Nimejifunza kwa njia ngumu sana kwa kufanya makosa yangu," anasema.

Unagundua haraka kwamba anajiamini sana utadhani ana kiburi. "Lakini kama kuna kitu ambacho ningebadilisha kwa watu watakaokuja baada yangu ni kupunguza ushuru."

Hebu tuzungumzie kazi yake nyingine - kuchanganya mvinyo. Kama angekuwa kinywaji cha kuchanganya angekuwa nini? "Ningekuwa Two Oceans. Ni kinywaji cha mseto wa gini na rumi." "Rumi ilitumiwa miaka ya 1860 kama pesa. Pia ilitumiwa kwa bidhaa za nywele. Rumi ilikuwa kila kitu. Kuna zaidi katika rumi kuliko inavyoonekana kwa macho." Kwa hivyo ni nini kimefichika ndani? "Ni shira tamu."

Atieno Otieno, ambaye alifanya kazi naye anaingilia. "Tazama, Pavraj ananifanya nihisi kama sijafanya chochote na maisha yangu. Huyu jamaa halali, halalamiki na hachelewi."

Nataka kuwaambia kwamba kukosa usingizi sio kitu kizuri lakini ananikatiza. "Kitu kimoja ninachojua kuhusu Pavraj ni kwamba atakupatia changamoto ya kutia bidii na kujipanga vyema. Anapoamua kufanya kitu, hima uko upande wake au unamzuia kukifanya. Ningekushauri kuwa upande wake au umuondokee."

Utafanya nini na watu kama Atieno, nani anataka washangiliaji? Furaha ni kama kipepeo: unapoifukuza, ndivyo inakimbia kwa kasi zaidi. Je, huwa anahisi furaha kabisa?

"Kama haujifurahii mwenyewe huwezi kufurahia chochote. Kila kitu ni kujikubali." Na kuhusu kujikubali, ananiambia kwamba anatatizika kupunguza uzito. Anajiandaa kwa mbio za marathon za Stanchart baadaye mwaka huu. Ule mkate wa burger aliokuwa akila mwanzoni hauonekani kuwa uamuzi mzuri.

# Sh1.6 bilioni

Pesa ambazo Wakenya walikopa kila siku kupitia Fuliza katika nusu ya kwanza ya 2022



**Pavraj Singh akiwa kazini katika kilabu jijini Nairobi.** PICHA | MAKTABA

Je, mambo yamekuwa shwari kwake? "Nikiwa na umri wa miaka 27, nilifikiria ningekuwa katika kazi ya kuketi ofisini. Au mpishi. Niko katika kilele cha kazi yangu na mambo yamekuwa bora zaidi. Kuna mengi ya kufuata na makosa ya kufanya. Natazamia kuona yatakayofanyika siku zijazo." Weita wetu Wafula anapojaza tena gilasi yake, ananiambia kuna kitu kimoja watu wanachokosea kila wakati kuhusu vinywaji. "Wanafikiria jinsi pombe yao itakuwa mchanganyiko mkali. Au jinsi wanaweza kuifanya iwe hivyo tena na tena. (Anajiandaa kwa shindano lake la kwanza. Atakuwa akitengeneza michanganyiko yake mitatu ya vinywaji.)

"Kuchanganya vinywaji kumenifunza nidhamu na uvumilivu. Ukiwa mtu wa sherehe na mtumiaji wa pombe, unatakiwa kudumisha utaalamu wako. Ukitaka ladha bora ya mvinyo, utasubiri kwa saa nyingi kabla ya kupata itakayokuridhisha. Kufikia sasa nimetayarisha tatu."

Licha ya mengi yake mazuri, ana mabaya pia. "Sijui kuhusiana vyema. Siwezi kudumisha mahusiano." Hata na Mungu. "Nikiwa kwa shida, ninajua Mungu atakuwa upande wangu."

Ni lini ulikosea Mungu mara ya mwisho? "Siku ya kuzaliwa. Unajua, siku yangu ya kuzaliwa ni sawa na ambayo Westgate ilishambuliwa. Nilikuwa nimealika marafiki kadhaa katika jumba hilo kwa karamu. Lakini gari langu lilikwama. Tulitumia saa tatu tukijaribu kulikwamua. Ni wakati huo ambao mama yangu alinipigia simu akaniambia nitazame habari. Siku hiyo nilipoteza marafiki wawili. Kama hakungekuwa na Mungu, ningekuwa hapa kweli?"

Kwa mara ya kwanza niliona ameingiwa na hofu. Anateremsha bia yake na ninaitisha burger yangu. Naam, bado anaendesha gari hilo. Naam, bado anafikiria alivyo na bahati. "Mambo yananiendea vyema hata wakati mwingine nashangaa, siri ni nini? Ni kama kufanya mkataba na shetani." Umefanya mkataba na shetani? "Hapana." Burger yangu inaletwa. Ninaiuma. Inaonja kama mbingu.

*eddyashioya@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

BIASHARA MPYA KATIKA MTANDAO WA KIJAMII

# UUNDAJI PODCAST: UTAJIRI UNAONUKIA

**UTUNZI WA MAUDHUI:** Ingawa inakua kwa haraka Afrika, podcast bado ni sekta inayoibuka. Kuendelea kutayarisha matukio bora kila wakati, kudumisha mapato na kujenga jamii si kitu rahisi

• NA SINDA MATIKO

Fikiria hili. Ukiwa na umri wa miezi miwili pekee, familia yako inahamia Uingereza kisha unarudi Kenya kwa ajali, miaka 27 baadaye. Naam, kwa ajali.

Ajali hiyo inakuwa mwanzo wa safari yako kama mtayarishaji wa podcast katika nchi inayostawi ambayo bado haijakumbatia podcast. Ukweli usemwe, utayarishaji wa podcast Kenya au Afrika, si kwa mtu dhaifu wa moyo, hasa wakati lengo ni kuifanya kuwa biashara.

Lakini hata ukifahamu haya vyema, hauvunjiki moyo. Unaamini, kutumaini na kuendelea mbele.

Unawekeza mamilioni kutimiza ndoto yako na kupata hasara kubwa. Unawekeza mamilioni ya pesa katika shughuli hiyo tena, lakini bado haupati faida kwa uwekezaji wako. Je, unaachana nayo?

Muundaji wa maudhui Eli Mwendwa sasa anaweza kutabasamu. Siku tunayoketi kwa mahojiano, uso wake unang'aa kwa tabasamu ya kupendeza na kuweka kila kitu wazi jinsi mcheshi wa Amerika Phyllis Diller alivyosema wakati mmoja. Hatimaye, kazi yake ya kutayarisha podcast imeanza kuzaa matunda.

Ni miaka mitatu tangu urafiki wake na wakili Oscar Koome uliposababisha kuibuka kwa moja ya podcast maarufu Kenya, Mantalk.ke, ambayo inajivunia kuwa na wasikilizaji 150,000. Mwezi jana, Mantalk.ke ilishida tuzo za African Podcast and Voice Awards.

"Baada ya kuishi Uingereza kwa miaka mingi ya maisha yangu, nilikuja Kenya kwa likizo na nikaipenda nchi hii. Niliamua kuanza biashara ya kuuza na kununua bidhaa nje ya nchi, ambayo ilifaulu vyema na hapo ndipo niliamua sitarudi Uingereza.

Nilianza pia kutayarisha maudhui ya dijitali, kwa ajali kabisa. Sikuwa na maisha ya kijamii kamwe, sikujua watu wengi na nilitaka kujuana na watu hapa. Hivyo ndivyo nilianza kuunda maudhui ya mitindo ya maisha, lakini pia kuyachapisha kwenye mtandao kwa marafiki wangu Uingereza waone ilivyo kuishi katika sehemu hii ya ulimwengu. Nilianza kupata wafuasi Kenya, kisha nikaanza kupata mialiko ambapo nilikutana na waundaji wa maudhui wanaojulikana.

Hapo ndipo niliamua kuwa muundaji wa maudhui na nikaanza kufanya kazi ya kupata hadhira," Mwenda anakumbuka.

Akiwa amelelewa katika nchi ambayo podcast ni maarufu, alihisi hii ilikuwa sehemu iliyohitaji kuchunguzwa. Mwanzoni hakupanga kuunda pesa kutoka kwa podcast zake.

"Nilipata kulikuwa na vitu hasi vilivyokuwa vikisemwa kwenye mtandao na nilitaka kuunda nafasi ambayo tungekuwa na mazungumzo chanya hasa kuhusu masuala ya wanaume. Nilikuwa nikiunda kundi jipya la marafiki na nikagundua tulikuwa tuking'ang'ana na masuala sawa nje ya mtandao. Kufikia sasa, imeendelea vyema sana. Ilinuiwa kuwa ya wanaume lakini sasa tuko na wanawake wengi wanaosikiliza na tukalazimika kujumuisha jinsia zote mbili."

Utayarishaji wa podacast ulianza aliyekuwa Dj wa video wa MTV Adam Curry alipotaka matangazo ya redio kwenye intaneti yaweze kupakuliwa moja kwa moja katika iPod yake. Kwa sababu hiyo, mnamo 2004, aliunda apu kwa jina iPodder; ikafanyiwa marekebisho machache na watengenezaji wachache na podcast kisha ikazinduliwa.

Watu walianza kufuatilia wakati podcast kuhusu makala ya habari ya upekuzi, Serial, ilivuma kote ulimwenguni. Ingawa bado si maarufu hapa nchini, podcast zinaanza kupenya katika soko la Afrika, hasa mijini.

"Wanaotumia podcast hasa wanapatikana katika miji mikubwa ya Kenya, Nigeria na Af-



Eli Mwenda: muundaji maudhui na mtangazaji mwenza wa podcast ya Mantalk.ke PICHA | MAKTABA

Nation Media Group "ePaper Copy"

kulingana na utafiti wetu, lakini hadhira inaongezeka katika miji mingine mikubwa katika nchi hizi tatu," anasema Josephine Karianjahi, Mkurugenzi Mwenza wa Africa Podfest, jukwaa la podcast barani. "Simu za mkononi ni vifaa muhimu vinavyotumiwa kupata podcast hasa kutokana na kupatikana kwa intaneti kupitia simu hizo na mitindo ya matumizi yake," anaongeza.

Licha ya umaarufu wake kuongezeka, bado ni vigumu kutumia podcast kupata pesa katika sehemu hii ya ulimwengu. Je, kuna pesa katika podcast Afrika? Ni swali lililoulizwa na Africa Podfest katika kongamano la ushirikiano na Siku ya Kimataifa ya Podcast.

"Tulifadhili Mantalk.ke wenyewe kwa miaka miwili ya kwanza. Sasa tunafanya kazi na chapa. Kabla ya hapo, tulikuwa tukipata hasara, kurudi kwa mifuko yetu au kupata pesa kutoka kwingine kufadhili mradi huo. Tangu tulipoanza, tumetumia karibu Sh2 milioni kwa Mantalk.ke."

Ingawa kuianzisha kunaweza kuonekana kitu rahisi, wanaume wawili wakiketi mbele ya maikrofoni kujadili masuala ya kijamii, gharama inategemea ubora na mfumo (sauti, video au zote mbili) wa podcast inayotayarishwa.

"Podcast bora ni ghali kiasi kutengeneza, lakini ni muhimu. Wazungumzaji ni mimi na Oscar, lakini huwa tunatafuta watayarishaji. Majuzi, tuliajiri mfanyakazi wetu wa kwanza, meneja wa mitandao ya kijamii,"

Kudumisha ubora na kuongezeka kwa hadhira kulithibitishia kampuni zinazowasaidia kuweka pesa katika podcast zao. "Mantalk.ke imeunda mfumo wake wa kipekee- podcast za sauti na video ambazo zinapatikana katika kila mtandao unaoweza kufikiria – kutoka Apple, YouTube, TikTok na Spotify hadi Afripods, Castbox, Instagram na Facebook. Kwa njia hii, tunaweza kushindana katika mitandao yote na kuwa na soko kubwa. Kwa hivyo kampuni inayokuja kwetu na pengine inataka kuweka tangazo katika Instagram, tunaweza kuonyesha kuwa tunaweza kuwapa zaidi kuliko tangazo au kuwataja katika mtandao mmoja," anaeleza Mwendwa.

Mantalk.ke imeanza kuuza nafasi za matangazo pia. "Kampuni nyingi zinaendelea kujua thamani ya podcast na hadhira inayotusikiliza na sasa tunaweza kuuza nafasi za matangazo, kama vile TV. Tunaweza kuuza kampuni, nafasi ya tangazo katika YouTube, TikTok au Instagram."

Hata hivyo, Eli anasema Mantalk.ke bado haijaanza kupata pesa nyingi inazofaa kuwa ikipata lakini anafurahishwa na hatua ilizopiga. "Podcast nyingi ng'ambo ni sauti tu na hazina hadhira kubwa kama Mantalk.ke. Lakini bado zinapata pesa nyingi kwa sababu biashara hiyo imestawi huko. Hatujafikia hapo kwa kupata pesa nyingi kutoka kwa matangazo ya sauti pekee kwa hivyo tulilazimika kutengeneza sauti na video."

Mtangazaji wa kituo cha redio cha Homeboyz na Deejay Conrad Gray, maarufu kama G Money, anakubaliana na hili. Podcast yake Mics Are Open, imekuwa ikifanya vyema tangu ilipozinduliwa Aprili 2019, kwani imechezwa mara 850,000.

Akishirikiana na Andy Young na Calvin Wanguku kuangazia maisha ya burundani, ucheshi na maisha, podcast hiyo kufikia sasa imewaletea zaidi ya Sh250,000 kupitia uuzaji wa bidhaa za podcast zilizopigwa chapa kama kofia, chupa na jezi.

Na kama Mantalk.ke ya Mwendwa, wamebahatika kupata matangazo ya kibiashara kutoka kwa kampuni kama Prudential Insurance, Safaricom na Adidas.

Lakini hii ilijiri kwa gharama kubwa. "Ufanisi mdogo ambao tunafurahia umekuja kwa gharama kama vile mabango na kampeni za dijitaji kutangaza podcast hiyo. Kuajiri mhariri wa video na mpigaji picha za video kumekuwa muhimu," G Money anasema (gharama ya kuweka tangazo katika bango Nairiobi ni kati ya Ksh100,000 na Ksh150,000, kulingana na eneo).

Kufikia Desemba 2020, podcast kwa jina Legally Clueless, ya aliyekuwa mtangazaji wa kituo cha redio cha Kiss 100, Adelle Onyang, Machi 2019, ilikuwa imepata hadhira ya watu 1.2 milioni. Legally Clueless ina matukio 112, ikichezwa mara 10,000 kwa wiki. Kama vile Mantalk.ke na Mics Are Open, inapatikana katika mitandao kadhaa kutoka YouTube, Facebook hadi IG TV, Apple, Soundcloud, Sticher, Tune-In na Spotify.

Mnamo 2020, Adelle alifaulu kufanya podcast yake kuwa ya kibiashara kuptia Trace FM, na kuwa podcast ya kwanza kufanya hivyo Afrika Mashariki.

Zaidi ya hayo, kwa usaidizi wa wafadhili na ushirikiano, Legally Clueless imeweza kupenya Senegal, Ghana, Ethiopia na Misri.


Hata hivyo, Adelle anakubali kuwa podcast Afrika inahitaji uwekezaji mkubwa na uvumilivu ili kufaulu. "Podcast zinakua kwa haraka upande huu wa ulimwengu, lakini bado ni sekta inayoibuka. Kuendelea kutayarisha matukio bora, kudumisha mapato na kujenga jamii si kitu rahisi," anasema Adelle.

Hata hivyo, Mwendwa ana matumaini kuhusu siku za baadaye za podcast barani Afrika. Mnamo Mei mwaka huu, Mantalk.ke ilwakilisha Kenya katika kongamano la Sounds of Africa lililoandaliwa na Spotify nchini Afrika Kusini ambako ruzuku ya Sh12 milioni kwa watayarishaji wa podcasts barani Afrika ilizinduliwa na tovuti hiyo.

"Tulianza tukiwa tumechelewa baada ya sehemu zingine za ulimwenguni lakini kuna pesa nyingi zinazomwagwa katika utengenezaji wa podcast Afrika kwa wakati huu. Baadhi ya mashirika hata yana idara za podcast. Tunaelekea pale Amerika na Uingereza zimekuw kwa muda," anasema.


***tmatiko@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*




ePaper Copy Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

tahariri




■ Kuna hofu huenda Rais William Ruto akakwepa katiba kwa manufaa yake ya kisiasa

Nation Media Group "ePaper Copy"

# Ruto anavyopalilia mamlaka yake Ikulu



KWENDO
OPANGA

Wakenya wameshuhudia yale ambayo Rais Ruto amefanya katika muda mfupi.

Amezuru Uingereza na Amerika, kisha Ethiopia, Uganda na Tanzania katika muda mfupi.

Dkt Ruto pia aliondoa ruzuku ya petroli na kupunguza bei ya mbolea kuonyesha kuwa atakuwa akitoa maamuzi mazito na kwa haraka.

Na kwa kupunguza riba inayotozwa mikopo inayopatikana kupitia simu, Rais ameonyesha anataka kuwajumuisha mama mboga, waendeshaji mikokoteni na wanabodaboda katika mpango wake wa kiuchumi wa kuwainua maskini.

Lakini baadhi ya makosa ambayo serikali hii imefanya yameibua hofu kuwa Rais Ruto ananuia kujilimbikizia mamlaka, kuwasamehe na kuwatuza washukiwa wa uhalifu huku akiuka katiba kwa manufaa yake ya kisiasa.

Siku chache baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais wa Agosti 9, Dkt Ruto alishawishi wabunge wa Azimio la Umoja-One Kenya kuhamia Kenya Kwanza.

Hatua hiyo ilipandisha ya hadhi mrengo wake wa Kenya Kwanza kuwa wa walio wengi katika Bunge la Kitaifa. Kuhama kwa wabunge wa Azimio kiliwezesha muungano huo kushinda waadhifa wa Spika wa Bunge la Kitaifa.

Siku moja baada ya Rais kuzuru ghafla majengo ya bunge, Spika Moses Wetang'ula alikabidhi Kenya Kwanza cheo cha Kiongozi wa Wengi licha ya pingamizi kutoka kwa wabunge wa Azimio.

Baada ya kulitia bunge mfukoni mwake, Ruto alikutana na mawaziri wanaoondoka, ambao baadhi yao walipinga azma yake ya urais. Mkutano huo ndio ulioondoa marufuku ya 2012 dhidi ya vyakula vinavyozalishwa kisayansi (GMO).

Marufuku hiyo iliondolewa bila maoni kutoka kwa umma, inavyohitajika kikatiba.

Hatua hiyo ilipingwa na makundi ya mashirika ya kijamii na vigogo wa Azimio; Raila Odinga na Kalonzo Musyoka. Makundi ya masharika ya kijamii yalifanya hivyo kwa kuegemea sayansi huku wanasiasa wakipaza sauti zao kupitia vyombo vya habari.

Ikumbukwe kuwa wakati wa kampeni, Ruto aliahidi mabadiliko na mambo mengi mazuri ndani ya muda mfupi. Hii ndiyo maana serikali yake tayari inamulikwa zaidi kuhusu utekelezaji wa ahadi zake chini ya miezi miwili baada ya kuingia ofisini. Hii ni tofauti kabisa na watangulizi wake.

Wananchi wanashinikiza serikali ipunguze bei ya petroli, unga na mafuta ya kupikia, miongoni mwa bidhaa zingine za kimsingi. Kwa jumla raia wanataka serikali ya Kenya Kwanza ipunguze gharama ya maisha.

Isitoshe wanasiasa wengine waliojiunga na Kenya Kwanza baada ya uchaguzi katika kilichoonekana kuwa hatua ya kuomba nyadhifa, hawana furaha kwa sababu hawajapata vyeo hivyo.

Lakini kile kimeibua maswali ni jinsi Rais Ruto na Naibu Rais Rigathi Gachagua wameingilia idara ya upelelezi wa jinai na kesi zinazowakabili wanasiasa.

Itakumbukwa kuwa Ruto alimkashifu vikali aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI) George Kinoti katika mikutano ya kampeni kwa kile alichodai kutumia ofisi yake vibaya.

Hata baada ya uchaguzi, Gachagua amekuwa akimlaumu Kinoti kwa kuongoza idara iliyojaa ufisadi na unyanyasaji. Hakuna aliyeshangaa kufuatia ripoti za Kinoti kujiuzulu. Wengi wanaamini alilazimishwa.

Ghafla, wanasiasa walioteuliwa mawaziri, na waliokabiliwa na mashtaka ya uhalifu walioondolewa mashtaka kabla ya kufika mbele ya kamati ya bunge kupigwa msasa. Bi Aisha Jumwa, aliyeteuliwa Waziri wa Utumishi wa Umma, alikabiliwa na kesi ya mauaji na wizi wa pesa za umma, ilhali Mithika Linturi, aliyeteuliwa Waziri wa Kilimo, alikuwa ameshtakiwa kwa ubakaji na ulaghai.

Waliondolewa mashtaka haraka, hatua ambayo iliibua maswali mazito. Imekuwaje kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma Noordin Haji? Aliwashtaki kwa mbwembwe kama kwamba alikuwa na ushahidi kwa kuhimili mashtaka na kuwapata na hatia. Aliondoa kesi hizo kimya kimya.

Hata hivyo, kwa kuondoa kesi dhidi ya wanasiasa hao, Haji amemhukumu Rais katika mahakama ya umma. Uamuzi wake ni rahisi. Akiwa na marafiki kama Bi Jumwa na Linturi, miongoni mwa washukiwa wengine wa uhalifu, Rais hahitaji maadui.

Lakini, hatimaye, baada ya Walio Wachache kutoa kauli zao, Rais Ruto, baada ya kuunda Walio Wengi, atafanya atakavyo.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Mteule wa Wizara ya Utalii, Wanyamapori na Turathi alinoa

# Shughuli ya kupiga msasa yageuka mzaha



MACHARIA **GAITHO**

Kwa muda wa wiki moja iliyopita tumekuwa tukifuatilia shughuli ya kupiga msasa mawaziri wateule wa Rais William Ruto.

Shughuli hiyo, ambayo imekuwa ikiendelea katika majengo ya Bunge, Nairobi, ilipeperushwa moja kwa moja na televisheni za hapa nchini.

Kupigwa msasa hadharani kwa mawaziri na maafisa wengine wakuu, wakiwemo wa Idara ya Mahakama, ni hitaji muhimu la Katiba ya sasa inayohimiza uwazi na uwajibikaji.

Shughuli hiyo hutoa nafasi kwa wabunge kudadisi walioteuliwa ili kubaini iwapo wanafaa au la. Wananchi nao hupata fursa ya kuwasilisha maswali na maoni yao kuhusu watu hao, kupitia taarifa kwa kamati inayoendesha shughuli hiyo.

Lakini suala moja ambalo lilijitokeza katika shughuli hiyo, iliyokamilika jana, ni kuwa ilikuwa mzaha na haikuzingatia malengo yake.

Naweza kuapa kuwa wote waliohojiwa wataidhinishwa kwa uteuzi rasmi, bila kujali kuwa baadhi yao hawafai kushikilia nyadhifa kuu serikalini. Tuliona wengine wenye viwango duni vya elimu kiasi kuwa hawafai hata kwa kazi ya karani. Lakini hivi karibuni ndio wataketi katika meza ya utungaji na utekelezaji wa sera za serikali kuu.

Kuna wengine ambao wanapaswa kuwa gerezani kwa tuhuma mbalimbali za uhalifu. Kwa kweli watu kama hao hawajatimiza viwango vya maadili yanayohitajika kwa washikilizi wa ofisi za umma, kulingana na Sura ya Sita ya Katiba. Lakini ajabu ni kuwa wote hawa watapita mtihani huo wa msasa "kwa alama za juu."

Hivi karibuni wafisadi hawa wote watakuwa wakipokea mishahara mikubwa na marupurupu, kutokana na pesa zetu za ushuru. Watakuwa wakibebwa kwa magari ya kifahari yenye vijibendera, wakizungukwa na wahuni huku wakihangaisha madereva wengine barabarani na kukiuka sharia za trafiki.

Suala muhimu katika shughuli ya kupiga msasa mawaziri wateule si maswali mazito yanayoulizwa, bali miegemeo ya kisiasa. Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula, Naibu Spika Gladys Boss Shollei, Kiongozi wa Wengi Kimani Ichungwa na wenzao wa Kenya Kwanza walioenekana kutetea wateule hao badala ya kuwadadisi kwa kina.

Wabunge wa Azimio, wakiongozwa na Kiongozi wa Wachache, Opiyo Wandayi na Kiranja wao, Junet Mohamed, walijaribu kuwadadisi wateule hao lakini juhudi zao hazikufaulu labda kutokana na kukosa habari na kutotaka au kutoweza kuuliza masuali magumu.

Suala lililofuatiliwa na wengi wakati wa shughuli hiyo ni utajiri wa wahojiwa, wote ni mamilionea na mabilionea wachache, jambo ambalo liliweka wazi uongo kuhusu serikali ya mahasla.

Lakini kuna baadhi walioonyesha ufahamu wa majukumu ya wizara wanazotarajia kuhudumia na wanayonuia kufanya. Hao ni Kipchumba (Uchukuzi, Barabara na Ujenzi) na Davis Chirchir (Kawi na Mafuta).

Wawili wanashikilia wizara zinazotajwa na Wakenya kuwa 'zenye faida' kutokana na bajeti kubwa zinazotengewa na nafasi za kuzipora kama ilivyoonekana chini ya serikali zilizotangulia.

Kwa sababu fulani, imekuwa desturi wizara kama hizo kuwekwa chini ya usimamizi wa 'vijana wa nyumbani'.

Hatutazungumzia sababu hizo kwa sasa, lakini kwa kuonyesha ufahamu kuhusu wanachonuia kufanya katika wizara zao, Murkomen na Chirchir pia walionyesha dalili kuwa watabadilisha sera na usimamizi wa mashirika chini ya wizara zao.

Kwa upande mwingine, Waziri Mteule wa Utalii, Wanyamapori na Turathi, Peninah Malonza, alionekana kutofahamu masuala muhimu ya wizara anayotarajia kuongoza. Hii ni licha ya umuhimu wa wizara hiyo kwa uchumi wa nchi kwa sababu huletea Kenya pesa nyingi za kigeni kila mwaka. Ni wazi kuwa Bi Malonza hana uwezo wa kuzungumza kwa ufasaha, sifa ambayo atahitaji ili kuvumisha Kenya kama kituo bora cha utalii.

**Suala lililofuatiliwa na wengi wakati wa shughuli hiyo ni utajiri wa wahojiwa, wote ni mamilionea na mabilionea wachache, jambo ambalo liliweka wazi uongo kuhusu serikali ya mahasla. Lakini kuna baadhi walioonyesha ufahamu wa majukumu ya wizara wanazotarajia kuhudumia na wanayonuia kufanya. Hao ni Kipchumba (Uchukuzi, Barabara na Ujenzi) na Davis Chirchir (Kawi na Mafuta).**

Lakini licha ya upungufu huo, ataidhinishwa kwa sababu mwishowe uamuzi huo hautafanywa kwa misingi ya uwezo wa mtu bali wingi wa wabunge wa Kenya Kwanza. Hii ndiyo maana tunafaa kutafakari upya kuhusu shughuli hii ya Bunge la Kitaifa ya kupiga msasa watu wanaoteuliwa kushikilia nyadhifa kuu serikalini.

Kama haitimizi lengo lililokusudiwa na walioandika Katiba ya sasa, ni heri tuitupilie mbali. Rais apewe nafasi na usemi wa kuteua anaowataka bila kuhitajika kuwasilisha majina yao Bunge wapigwe msasa.

Jinsi nyingine ni kuondoa shughuli hiyo mikononi mwa wanasiasa bungeni na kuipa asasi huru ambayo haiwezi kushawishiwa na Rais, chama fulani cha kisiasa, kinachounga mkono serikali au chama cha upinzani.

Mwishowe, kuna suala lililojitokeza katika shughuli hiyo ambalo linafaa kutajwa hapa. Kwamba kila aliyependekezwa kuwa waziri ametoka familia masikini, alienda shule bila viatu na wazazi wake walikuwa na wakati mgumu kuwalisha na kuwalipia karo ya shule. Baadhi yao walikatiza masomo wakati mmoja kwa kukosa karo. Ajabu ni kuwa hata mamilionea walilazimika kubuni hadithi kuonyesha kuwa awali walikuwa mahasla lakini wamebadilisha maisha kutokana na bidii yao, kwa hivyo wana haki ya kuhudumu katika serikali ya Kenya Kwanza.

*** ***

Kwa mara nyingine, Naibu Rais Rigathi Gachagua, ameachilia ulimi wake tena. Wiki iliyopita, alizua malalamiko tena kwa tangazo lake kuwa amri za mahakama kuhusu watu kutimuliwa, kwa mfano, hazitatekelezwa bila idhini ya kamati za usalama katika maeneo yanayohusika.

Labda hilo ni muhimu katika juhudi za kudumisha amani, lakini pia kwa tangazo hilo, Naibu Rais aliidhinisha jaribio la kijinga na haramu la Kamati ya Kitaifa ya Usalama la 'kubadilisha' matokeo ya uchaguzi wa rais ambayo yaliiweka serikali ya sasa mamlakani. Inaitwa mantiki.

**gaithomail@gmail.com**

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ KUTENGANISHA MAMLAKA

# MAWAZIRI KATIKA BUNGE

*Rais Ruto atategema wabunge kufanyia mageuzi Kanuni za Bunge ili kuruhusu Mawaziri kuhudhuria Bunge kuwasilisha msimamo wa serikali kila wanapohitajika kufanya hivyo*

● NA HAMMERTON MALOBA

Mpango katika manifesto ya kampeni ya Rais William Ruto wa kubadilishwa kwa Kanuni za Bunge ili Mawaziri wawe wakifika bungeni kuulizwa maswali inaweza kubadilika kuwa kiazi moto kisiasa.

Juhudi sawa mnamo 2014 zilizimwa aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta alipokataa kutoa idhini kwa msingi kuwa itaenda kinyume na shabaha ya katiba ya kutenganisha mamlaka.

Masuala kama hayo yataibuka iwapo serikali ya Kenya Kwanza itatoa pendekezo hilo tena, na maswali zaidi yanaweza kuibuliwa kuhusu kujitolea kwa Ruto na heshima yake kwa kanuni za kimsingi.

Kwa mfano, Ruto, ameashiria kuwa njia itatafutwa kuruhusu wabunge kupata pesa za Hazina ya Maendeleo ya Maeneo Bunge (CDF), ambayo Mahakama imesema inakiuka katiba kwa sababu wanachama wa mhimili wa Sheria wa serikali hawawezi kusimamia moja kwa moja matumizi ya pesa wanazopaswa kuwa wakipiga darubini.

Serikali ya Jubilee ya aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta, ambayo Ruto alikuwa Naibu Rais, ilijaribu sana kukwepa muundo wa sheria kwa kubatiza CDF ilipoipatia jina la Hazina ya Serikali ya Kitaifa ya Maeneo Bunge, lakini Mahakama haikuona tofauti yoyote.

Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula amekuwa akiongoza ukaidi dhidi ya hatua ya Tume ya Kutathmini mishahara ya kuzima Marupurupu mengi ambayo wabunge hutumia kuongeza mishahara yao.

Hakuna dalili kuwa Ruto, ambaye amewataka Wakenya wakaze mishipi, na kupunguza matumizi ya kila aina kutokana na hali mbaya ya bajeti, yuko tayari kuwazima wabunge. Badala yake, anatoa ishara za kuundwa kwa hazina nyingine ya Maseneta, ambayo inasemekana ni ya kutumiwa kupiga darubini matumizi ya pesa katika serikali za kaunti.

Katika serikali iliyoondoka, Ruto aliongoza upinzani dhidi ya mageuzi ya katiba ya Mpango wa Maridhiano yaliyofadhiliwa na Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga. Sababu kuu za kukataa mapendekezo hayo zilijumuisha kutumiwa kwake kwa shughuli za kisiasa kuunda wadhifa wa Waziri Mkuu. BBI ilishindwa, lakini Ruto pia aliunda wadhifa wa Mkuu wa Mawaziri kwa ajili ya mshirika wake katika muungano wa Kenya Kwanza, Musalia Mudavadi.

Maswali yameulizwa kuhusu uhalali wa wadhifa huo kwa kuwa katiba inatambua Rais na Naibu Rais pekee katika Ofisi Kuu ya Rais.

Malalamishi yalikomeshwa, hata hivyo, kwa sababu Kiongozi wa Upinzani Raila Odinga pia alikuwa amependekeza wadhifa wa Mkuu wa Mawaziri kwa mshirika wa muungano wake, Kalonzo Musyoka. BBI, ambayo Ruto alikataa, pia ilipendekeza mfumo ambapo Mawaziri wangeteuliwa kutokana na wabunge wanaohudumu, ilivyokuwa chini ya katiba ya kabla 2010, pia kinyume na shabaha ya kutenganisha mamlaka.

Je, Mawaziri watahudhuria vikao vya bunge kujibu maswali? Mnamo Juni 11, 2014 na Agosti 28, 2014, wabunge walikubali mapendekezo ya kuruhusu Mawaziri kufika bungeni, na wakabadilisha Bunge kuwa Kamati Kuhusu Usimamizi kupokea majibu ya maswali. Hata hivyo, mabadiliko haya hayakudumu kwa muda mrefu. Rais Kenyatta aliandikia Bunge kulikumbusha kuhusu katiba mpya inayokitwa kwa msingi wa kutenganisha mamlaka kwa mujibu wa Ibara 153(3).



Waziri Mteule wa Mazingira na Misitu Roselinda Soipan Tuya akizungumza katika Hoteli ya Serena, Nairobi, Oktoba 1.

Alisema Kanuni Mpya za Bunge zilikiuka usawazishaji tete kati ya Serikali Kuu na Bunge. Rais alihimiza Bunge lisitishe utekelezaji wa kanuni hizo mpya na kuwazia kuzifanyia mabadiliko ambayo yangezingatia kutenganisha mamlaka.

Kwa hilo, shughuli za Kamati Kuhusu Usimamizi zilisitishwa. Bunge liliokolewa na sehemu katika kanuni hizo iliyotoa nafasi kwa Mawaziri kufika mbele ya Kamati za Bunge kujibu maswali. Ni kupitia mpango huu ambapo Mawaziri walifika mbele ya kamati tofauti za Bunge. Kulingana na Rais Ruto, wakati umefika wa kutumia mbinu tofauti.

Ili Bunge liweze kutekeleza majukumu yake vyema ya kupiga darubini Serikali Kuu, ni lazima ipewe nguvu za kuwaita Mawaziri ndani ya Bunge kuulizwa maswali.

Kwa kufanya hivyo, Rais atategemea Wabunge kufanyia mageuzi Kanuni za Bunge kuruhusu Mawaziri kufika bungeni kuwasilisha msimamo wa serikali wanapohitajika kufanya hivyo.

Hata hivyo, kizungumkuti hapa kitakuwa jinsi ya kuafikia usawazishaji tete kati ya haja ya kuwa na serikali iliyoungana kukiwa na mahitaji ya katiba ya kutenganisha mamlaka kati ya Serikali Kuu na Bunge. Kuna uwezekano mkubwa kwamba wabunge wataanzisha upya mabadiliko yaliyosimamishwa na Bunge la 11 yakiwa na mageuzi machache.

Mageuzi ya Kanuni za Bunge yanaweza kuanzishwa mara moja na Kamati ya Taratibu na Sheria au na mbunge binafsi akiungwa mkono na wabunge wasiopungua 50. Katika hali hizi mbili, Kamati ya Taratibu na Sheria za Bunge inachunguza ombi lililoandikwa la kupendekeza mageuzi hayo. Ombi hilo huwa na maelezo ya kuhalalisha mageuzi yaliyopendekezwa, ambayo ni lazima yawe na majina na saini za wabunge wanaounga mkono ombi hilo. Baadaye linawasilishwa kwa Spika ambaye, baada ya kuridhika linatimiza mahitaji yaliyotajwa hapa juu, analituma kwa Kamati ya Taratibu na Kanuni za Bunge lijadiliwe. Kamati hiyo huwa na siku 21 kulijadili na kuwasilisha ripoti kwa Bunge.

***Bw Maloba ni Wakili wa Mahakama ya Juu Kenya***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

SIFA ZINAPOZIDI HALI HALISI

# GATUNDU: KISA CHA UKWELI NA UONGO

*Sio eti eneobunge hilo ambalo limetoa marais wawili - baba na mwanawe, katika muda wa miaka 34 – lina watu wazembe; ni vile tu wamekosa uongozi*

NA MAGESHA NGWIRI

Kwa muda mrefu katika historia ya nchi hii kama taifa huru, barabara zote zilisemekana kuelekea Gatundu. Hii ni kwa sababu rais wa kwanza wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta alitoka kata hiyo katika Wilaya ya Kiambu, na mtu yeyote aliyehitaji kukutana naye, katika kikao rasmi au kisicho rasmi, alilazimika kusafiri hadi nyumbani kwake kijijini wakati rais hakuwa na shughuli rasmi jijini Nairobi. Kutokana na sababu ambazo hazijawahi kueleweka, alikuwa akisafiri kila siku kati ya Ikulu na kijiji cha Ichaweri kilicho umbali wa kilomita 32 kutoka Nairobi.

Kuanzia 1964, ilikuwa furaha ya wanafunzi kupanga foleni kando ya Barabara ya Kenyatta kumsubiri rais wao kwenda nyumbani jioni akisindikizwa na sauti za ving'ora na mataa yaliyoangaza. Angepokea salamu zao kwa kupungia mwengo wake maarufu, kisha kuondoka. Wavulana waliosubiri kwenye foleni kushangilia sasa ni wazee wa kuheshimika, lakini itakuwa vigumu kwao kusema ni kitu gani walichokuwa wakisherehekea. Leo hii, ni wachache sana wanaoweza kutaja ni kitu gani hasa walichotendewa na Mzee Kenyatta alipokuwa mbunge na rais wao kwa miaka yote hiyo.

Tangu enzi za ukoloni, Kaunti ya Kiambu ilikuwa na mashamba makubwa ya majani chai na kahawa yaliyomilikiwa na wazungu. Wakulima wengi waliingiwa na hofu baada ya uhuru, wakauza mashamba yao na kuondoka. Hiyo ndiyo sababu hakuna waliobakia katika maeneobunge ya Gatundu Kusini na Kaskazini. Tetesi zinasema baadhi ya wakulima walishinikizwa kuuza ardhi zao lakini hilo si rahisi kuthibitisha. Katika muda wa chini ya miaka mitano, mengi ya mashamba yalikuwa mikononi mwa Wakenya mabwanyenye ilhali maisha ya raia wa kawaida hayakubadilika.

Isitoshe, Mzee Kenyatta, kinyume na mrithi wake, Rais Moi, alitilia maanani zaidi ujenzi wa shule za msingi na za sekondari. Lakini imeibuka kuwa alitaka chuo kikuu kijengwe katika kijiji cha Mutomo, umbali wa kilomita moja kutoka nyumbani kwake. Kwa bahati mbaya, mpango huo ulipingwa na wazee wa jamii. Badala yake Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Sayansi na Teknolojia (JKUAT), kilijengwa mjini Juja. Sasa imeibuka kuwa Chuo Kikuu cha Mama Ngina kinajengwa eneo hilo. Kwa kuwa historia hujirudia, hatua hii pia inapingwa kortini na watu wasiotaka kuachilia ardhi yao.

Kisa cha Gatundu kinakanganya, kwa kuwa sifa yake hailingani na uhalisia. Maeneobunge hayo mawili (ambayo sasa ni kauti ndogo za Kiambu) hayawezi kujigamba kwa maendeleo yoyote ya kipekee. Huenda si maeneo fukara zaidi, kwa sababu yanatoka katika kaunti ya pili tajiri zaidi Kenya, lakini huwezi kujua kwa kuzingatia kuwa pengo kati ya matajiri na maskini linaonekana kuzidi kupanuka.

Ikiwa na wakazi karibu 700,000, Gatundu ni eneo lenye idadi kubwa ya watu, na wengi wao wanamiliki vipande vidogo vya ardhi. Huwa wanategemea kilimo cha kinachotegemea mvua kukuza tu chakula cha kujikimu.



Mzee Jomo Kenyatta

Hata hivyo, ni viongozi wachache sana, kuanzia rais wa kwanza, madiwani, wabunge, magavana au rais wa nne, wamewashauri kuhusu jinsi ya kutumia kikamilifu vipande hivyo vidogo vya ardhi (ekari 0.7 kwa wastani) ili kuboresha maisha yao. Sio eti eneobunge hilo ambalo limetoa marais wawili - baba na mwanawe, kwa miaka 34 – lina watu wazembe; ni vile tu wamekosa uongozi. Hakuna viwanda vya kutayarisha bidhaa za kilimo licha ya kuwa wakulima hukuza mazao ya kutosha kama vile ndizi, mananasi, parachichi na macadamia yanayohitaji viwanda kama hivyo.

Sasa watu wa Gatundu waliopigia kura serikali mpya kwa moyo wao wote wanatumai kwa dhati kutakuwa na mabadiliko katika maisha yao. Kulingana na kiongozi mmoja wa jamii, hawakumpigia kura Rais William Ruto kwa sababu walimchukia Raila Odinga; walikuwa wanapiga kura dhidi ya Rais Uhuru Kenyatta kwa sab bu alikuwa amewatelekeza kwa muda mrefu sana, kisha alikuwa na ujeuri wa kuwaambia wamchague Raila.

Uasi huu una historia ndefu. Mnamo 1997, Bw Kenyatta alipogombea kwa mara ya kwanza kiti cha ubunge Gatundu Kusini, alishindwa na mgombeaji ambaye si wengi waliomjua kupitia njama kali aliyochezewa na mahasidi wake. Alichaguliwa mbunge kati ya 2002 na 2013, lakini haikuwa na maana vile kwa sababu uwakilisha wake haukuleta mradi wowote maalumu wa maendeleo uliohusishwa naye. Hasa, alizoea kuwaudhi wengi kwa kuwaachia jamaa za familia yake kumwakilisha katika majukumu ya ubunge yanayochosha zaidi.

Kosa alilofanya, safari hii kama rais, lilikuwa kupuuza ushauri kutoka kwa wazee wa jamii, ambao wangemueleza kilichokuwa kikitokota kisiri. Kama alijitenga alipokuwa mbunge, akiwa rais alitoweka kabisa na kuwa asiyeweza kufikiwa kamwe. Kwa sababu hiyo hakuweza kugundua watu walikuwa wanamuondokea na kuweka matumaini yao kwa mtu aliyekuwa akiahidi mabadiliko. Kama mtu mwenye maarifa katika mambo mengi, alifaa kukumbuka huenda msemo "ukarimu huanzia nyumbani" umerudiwa sana, lakini ni wa kweli.

Pigo la mwisho lilikuwa Bwawa la Karimenu II ambalo alizindua siku nane tu kabla ya utawala wake kufika kikomo. Bwawa hilo lililogharimu Sh24 bilioni eneo la Gatundu Kaskazini, kwa kuzingatia haki, linafaa kusambaza maji kwa wakazi eneo hilo, lakini imegeuka kuwa maji hayo yananuiwa kufaidi miji iliyo katika mkondo huo ikiwemo Juja, Ruiru, kampuni ya maziwa ya Brookside Dairy inayomilikiwa na familia ya Kenyatta na shirika lingine la familia hiyo la Northlands City. Hilo, bila shaka, liliwaudhi wakazi wa Gatundu ambao kwa muda mrefu wameishi bila maji safi ya mfereji.

Na kwa wananchi walioambiwa kuna ofisi iliyojengwa na Jomo na kufanyiwa ukarabati na Uhuru ambako pesa humwagwa mara kwa mara kwa wakazi, hiyo si kweli. Idadi kubwa ya raia wa eneo hilo ni walalahoi wanaotegemea jasho lao kupata riziki, na ndiyo maana ujumbe wa hasla uliteka nafsi zao. Matokeo ni kuwa kushindwa huku kwa mwisho huenda kukawa mwisho wa utawala wa familia ya Kenyatta katika siasa za Gatundu. Lakini pia, chochote chaweza kutokea katika siasa.

***andrewngwiri@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Darubini mpya yatatua fumbo kuhusu nyota iliyojaa vumbi

Ni moja kati ya picha za kipekee zilizoonekana kutoka kwa darubini mpya ya kisasa kwa jina James Webb. Watu wengi walishangaa ilipowekwa kwenye mitandao ya kijamii mwishoni mwa Agosti.

Hata hivyo, wanaanga walifurahi sana kutokana na maelezo ya kina waliyopata. Picha hizo zinaonyesha WR 140. Ni nyota nadra sana. Pete hizo ni makundi ya vumbi, yenye upana wa hadi kilomita trilioni kumi. Huo ni umbali mgumu sana kuelewa.

Kwa njia nyingine, ina upana mkubwa mara 70,000 ya umbali uliopo kati ya Dunia na Jua. "Mitazamo ya awali ya WR 140 ilifichua kuwepo kwa hadi pete tatu. Ni hali inayoonyesha nguvu ya James Webb," akasema Dkt Olivia Jones kutoka Kituo cha Tekinolojia na Uanaanga cha Uingereza, jijini Edinburg.

Kituo hicho kilisaidia sana kwenye ujenzi wa darubini hiyo. WR ni ufupisho wa "Wolf Rayet", aina ya nyota kubwa. Nyota hizo hutoa pepo kali za gesi angani. Hii ina uzito unaozidi jua mara 30. Inakisiwa nyota hizo ni 10 pekee angani zima. Mienendo yake ndiyo huzalisha vumbi. Pepo hizo hufinyana na kutengeneza vumbi. Ajabu ni kuwa vumbi hutokea kwa kiwango kikubwa nyota hizo zikikaribiana na zinapoelekea pande tofauti. Hilo linaeleza chanzo cha taswira yake ya kushangaza kulingana na picha zilizopigwa na James Webb. Wanaanga wameeleza kushangazwa na uthabiti mkubwa wa nyota hizo. "Tunatazamia mfumo huu utaendelea kutoa vumbi kwa karne moja ijayo," akasema Dkt Ryan Lau kutoka maabara ya Wakfu wa Kitaifa wa Sayansi, Amerika, NOIRLab.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# SPIKA ZA MASIKIONI ZA KAWI YA JUA NI LAZIMA



LONDON

Kama wewe ni mtu alyezoea kusahau kuweka moto spika za masikio zisizokuwa na waya, huenda hatimaye ukapata afueni. Sasa unaweza kununua spika za kwanza za masikio zinazopata moto kupitia kwa jua.

Zimeundwa na kampuni za Urbanista na Addidas kutoka Sweden na Ujerumani mtawalia. Sehemu za kuingiza moto zimetengenezwa na kampuni ya Exeger kutoka Sweden pia. Kampuni hiyo imechukua karibu miaka kumi kuzitengeneza ili kulingana na mahitaji la kisasa.

Mkuu wa Exeger, Giovanni Fili, anasema muundo huo unasaidia spika hizo kubebeka kwa urahisi na kuhifadhi mazingira. "Kila mtu anachukia kuweka moto vifaa hivi," anasema. "Lakini kila wakati unapoweka moto bila kutumia umeme, ni manufaa makubwa kwa dunia nzima. "Kizazi cha sasa kinatarajiwa kupewa vifaa kuhifadhi mazingira, na hivyo ndivyo tunavyofanya."

Vifaa vya kutega kawi ya jua vya kampuni ya Exeger vinaitwa Powerfoyle na vina upana wa milimita 1.3. Tekinolojia yake imejengwa kwa madini aina ya titanium dioxide.

Spika hizo pia zina betri inayoweza kukaa hadi masaa 80. Ni betri hiyo inayowekwa moto kwa tekinolojia ya Powerfoyle. Fiji anasema tekinolojia hiyo ina uwezo wa kubuni umeme utakaotumika kwa saa moja bbada kuwekwa juani kwa dakika 20 pekee.

Paneli hizo pia zina uwezo wa kutengeneza kawi kutoka kwa mwanga wa kawaida. Hilo linamaanisha kuwa spika hizo hujiweka moto kila wakati, isipokuwa tu zinapokuwa kwenye giza. Isitoshe, zina eneo mbadala la kuwekea moto, ikiwa moto uliowekwa umeisha na hakuna njia nyingine ya kuweka moto mwingine.

Fili anaongeza huenda paneli hizo zisiwekwe katika simu za rununu, kwani watu wengi hubeba simu hizo mifukoni, kumaanisha haziwezi kupata mwanga. Badala yake anasema huenda zikawekwa katika nguo za watu au mikoba, ili kuweka moto simu hizo.

Tayari, kampuni ya Planno kutoka Finland inatengeneza vitambaa vilivyo na muundo wa paneli za kawi ya jua. Kampuni hiyo inaongozwa na Elina Ilen, ambaye pia ni profesa katika Chuo Kikuu cha Polytechnic Catalonia, Idara ya Nguo na Uhandisi wa Karatasi.

Badala ya kutengeneza nguo zinazoweza kuweka moto simu yako ya rununu, kampuni hiyo inanuia kutengeneza nguo zenye uwezo wa kukusanya kawi kulingana na mazingira ya aliyezivaa. Mavazi yanaweza kudhibiti mambo tofauti ya aliyevaa, kama kasi ya mpigo wa moyo wake, kiwango cha joto, alivyolala na kiwango cha mafuta katika mwili wake.

"Ingawa seli hizo za kawi huwa hazizalishi kawi ya kutosha, kuziweka katika nguo hakuwezi kulinganishwa na kiwango cha kawi kinachoweza kupatikana zikiwekwa kwenye jua," akasema Ilen.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ VITA VYA NDANI ETHIOPIA: FISI WAPATA KITOWEO



Wakimbizi wa Ethiopia waliotoroka vita katika eneo la Tigray wakibeba mitungi ya maji katika kambi ya Umm Rakuba, jimbo la Gedarefin, mashariki mwa Sudan, mnamo Agosti 11, 2021.

# MAISHA YA JEHANAMU TIGRAY

*Wakati mmoja eneo hilo lilikuwa kivutio cha watalii, wageni wakivutiwa na makanisa yaliyochongwa kwenye miamba, maeneo matakatifu ya Waislamu na maandishi ya zamani kwa lugha ya Ge'ez. Sasa Tigray ni eneo la vita vikali huku wanajeshi wa Ethiopia na Eritrea upande mmoja, na wapiganaji wa Tigray People's Liberation Front (TPLF) upade mwingine, wakipigania udhibiti wa eneo ambalo kwa muda mrefu limeonekana kuwa muhimu kwa mamlaka nchini Ethiopia - au iliyokuwa sehemu ya Abyssinia*

● ADDIS ABABA

Fisi wanakula maiti za wanakijiji, miji mikubwa na midogo inashambuliwa kwa makombora yanayorushwa kutoka angani huku wazee na wanawake wakisajiliwa katika makundi ya wapiganaji - haya ndio maelezo na taswira ya kuhofisha kutoka kwa vita ambavyo vimesababisha vifo vya maelfu ya watu katika eneo la kihistoria la Tigray, nchini Ethiopia.

Eneo hilo wakati mmoja lilikuwa kivutio cha watalii, wageni wakivutiwa na makanisa yaliyochongwa kwenye miamba, maeneo matakatifu ya Waislamu na maandishi ya zamani kwa lugha ya Ge'az. Sasa Tigray ni eneo la vita vikali huku wanajeshi wa Ethiopita na Elitrea upande mmoja, na wapiganaji Tigrays People's Liberation Front (TPLF) upande mwingine, wakipigania udhibiti wa eneo ambalo kwa muda mrefu limeonekana kuwa muhimu kwa mamlaka nchini Ethiopia – au

Shughuli zimekwama eneo hilo kwa miezi 17 - hakuna huduma za benki, simu au intaneti - na halifikiwi na wanahabari. Mnamo Novemba 2020 wanajeshi wa Ethiopia na Eritrea walishambulia mji mkuu wa Tigray, Mekelle, baada ya wapiganaji wa TPLF kudaiwa kushambulia kambi ya wanajeshi wa Ethiopia. TPLF ilifanya mashambulio ya kulipiza kisasi katika maeneo jirani ya Amhara na Afar, huku wakikaribia jiji kuu Addis Ababa mwaka mmoja baadaye.

Katika mapigano ya hivi majuzi, wanajeshi wa Ethiopia na Eritrea walishambulia mji wa Shire wakionyesha dalili za kutwaa usimamizi wa mji wa Mekelle kwa mara nyingine."Jumla ya wanajeshi 500,000 wa Eritrea na Ethiopia wako vitani eneo hilo, pamoja na wapiganaji wengine 200,000 kutoka upande wa TPLF," akasema Alex de Waal, mkurugenzi mkuu wa Wakfu wa Kutetea Amani Ulimwenguni (World Peace Foundation), wenye makao yake nchi Amerika.

Aliongeza kuwa baada ya zaidi ya siku 50 za vita mfululizo, wiki hii wapiganaji wa TPLF mjini Shire walilemewa baada ya kuishiwa na risasi. "Ni pigo kubwa kwa wapiganaji wa Tigray. Vimeweka raia katika hatari ya kuuawa, kubakwa na kuathiriwa na baa la njaa," Profesa De Waal alisema. Hii ni licha ya kuwa serikali ya Ethiopia imeahidi kupeleka msaada wa chakula na kurudisha huduma muhimu mjini Shire na maeneo mengine yaliyo chini yake.

Hali inayoshuhudiwa Shire inaakisi changamoto za kibinadamu katika jimbo la Tigray, huku jumla ya raia 600,000 wakifika mjini humo kutafuta uhifadhi baada ya kutoroka maeneo mengine yanayokumbwa na vita. "Watu Zaidi 120,000 hawana makao, wanalala chini ya miti na misituni," akasema mfanyakazi wa shirika la kutoa misaada, aliyeomba tusitaje jina lake.

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya afrika

# Fisi wala maiti za wanaouawa vitani Tigray

Kutoka Uk 25

Karibu wafanyakazi wote wa kutoa misaada waliondoka Shire wiki chache baada ya mji huo kushambuliwa na wanajeshi wa Ethiopia. Maelfu ya raia walitoroka Shire wakihofia dhuluma.

"Mashahidi wanne waliripoti kuwa watu 46 walishambuliwa na kuuawa katika kijiji cha Shimblina mnamo Septemba. Maiti za zilipatikana zimechanganyika na mizoga ya mifugo ambao pia waliuawa," mfanyakazi huyo wa shirika la kutoa misaada akasema.

"Baadhi ya maiti zilikuwa zimeliwa na fisi na zilitambuliwa kwa mabaki ya mavazi. Mkazi aliyeshuhudia mauaji hayo alisema hawakuwa na nafasi ya kuzika maiti hizo na huenda fisi wamewamaliza kufikia sasa," akaongeza.

Wengi wa waathiriwa wa mapigano hayo ni watu wa kabila dogo la Kunama, ambalo halihusiki katika mapigano hayo. "Pande zote mbili zinapoteza wanajeshi wake katika mapigano na ndiyo maana wakifika vijijini wanaelekeza hasira zao kwa wenyeji," akaongeza.

Wapiganaji wa TPLF pia wanalaumiwa kwa maovu sawa - ubakaji, uporaji wa mali na muaji ya raia kiholela - waliposhambulia maeneo ya Amhara na Afar. Baadaye walisukumwa na wanajeshi wa Ethiopia na kurudishwa Tigray. Eneo hilo lina jumla ya wakazi milioni saba, idadi ndogo ikilinganishwa na watu milioni 100 wa nchi nzima ya Ethiopia.

Kando na vitendo vya ukatili, wanajeshi wa serikali na wapiganaji wa TPLF wote wamelaumiwa kwa kusajili raia kusaidia vitani. "Watu wanasajiliwa na baada ya mafunzo ya wiki chache wanapelekwa vitani kukabiliana na adui," akasema Abdurahaman Sayed, mchanganuzi wa shirika la kufuatilia masuala ya usalama katika Upembe wa Afrika.

"Adui anashambulia na kuua wengi wao. Lakini wanaendelea kufika kwa makundi hadi adui anaishiwa na risasi. Kisha wanatwaa eneo hilo. "Ni mbinu ya zamani ya kivita. Ilitumiwa kwa mara ya kwanza na mfalme wa Abyssinia dhidi ya wavamizi wa Italia miaka ya 1890. Licha ya kuwa na silaha za kisasa, Wataliano walilemewa kutokana na idadi kubwa ya watu waliowakabili," Abdurahman akasema.

Alisema mbinu hii husababisha mauaji ya watu wengi ikadiriwa kuwa kati ya 700,000 na 800,000 wameuawa tangu vita hivyo vipoanza miaka miwili iliyopita. "Hivi ni vita vibaya zaidi katika historia ya Ethiopia," akaongeza.

Ingawa mchanganuzi wa masuala ya Upembe wa Afrika, Faisal Roble, anayeishi Amerika, alipinga madai kuwa wapiganaji wa Tigray walitumia raia katika vita hivyo, takwimu kuhusu waliouawa hazikuwa na tofauti kubwa. "Katika awamu mbili za kwanza za vita hivyo, watu 500,000 walikufa na watu 100,000 walikufa katika awamu ya tatu," akasema.

Roble aliongeza kuwa wanajeshi wa Tigray walikuwa wamepokea mafunzo ya kivita, lakini wanajeshi wa Ethiopia waliwalemea kwa idadi na uwezo wa mashambulio ya angani.

"Jenerali ambaye sasa ni balozi alisema wangeweza kusajili vijana milioni moja kila mwaka katika jeshi. Pia wana ndege za kivita na droni kutoka Uturuki ambazo ni bora zaidi vitani. Wanajeshi wa Tigray hawana zana za kufanya mashambulio ya angani," akasema.

Kikosi cha jeshi la angani la Ethiopia kilipelekwa katika jiji kuu la Eritrea, Asmara, ambako ndege zake za kivita zilikuwa zikianzia safari, akasema Roble. Hii ni kwa sababu mji huo unakaribiana na eneo la Tigray kuliko kituo cha kawaida cha wanajeshi hao mjini Bishoftu, eneo la kati mwa Ethiopia.



Eshete Zewudru (kulia) mpiganaji wa kundi la wanamgambo la Amhara Fano, abusu msalaba ulioshikwa na kiongozi wa dini ya Orthodox Ethiopia katika kanisa lililochongwa kwenye mwamba, eneo la Lalibela, mnamo Disemba 7, 2021.

Eritrea iliingilia kati vita hivyo kwa sababu ni adui wa kundi la waasi wa TPLF. Wanachama wa TPLF walihudumu katika serikali ya muungano Ethiopia hadi Waziri Mkuu wa sasa, Abiy Ahmed, alipoingia uongozini 2018.

Chini ya TPLF, Ethiopia na Eritrea zilishiriki vita vya mpakani ambako karibu watu 80,000 waliuawa. Baadaye, mahakama ya kimataifa ilitoa uamuzi kuwa Ethiopia inafaa kukabidhi eneo hilo kwa Eritrea. Lakini serikali iliyodhibitiwa na TPLF ilikataa. Eritrea ilitwaa tena eneo hilo baada ya vita vya Tigray vilivyoanza Novemba 2020.

Wakosoaji wa nchi hiyo wanasema Rais Isaias Afwerki amejitolea kusaidia Bw Abiy kumaliza kundi la TPLF ili lisitishe taifa lake (Afwerki). "Eritrea inahofia TPLF linataka aidha kutwaa uongozi kutoka kwa serikali ya Ethiopia au kusimamia eneo fulani nchini humo ili kulitumia kufikia bahari ya Red Sea kwa sababu Tigray haiko karibu na bahari na ni masikini," akasema Abdurahman.

Huku vita Tigray vikichacha katika wiki chache zilizopita, serikali ya Eritrea imeanza kuandaa wanajeshi wake kwa mashambulio. Katika tukio moja Septemba, wanajeshi wa Eritrea walivamia kanisa kusini mwa mji wa Akrur, eneo la Tigray. Duru zinasema kasisi, waumini na wanachama wa kwaya walizuiliwa kwa kukaidi matakwa ya wanajeshi.

Profesa De Waal alisema maandalizi hayo ya wanajeshi yanaonyesha kuwa Bw Isaias anachukua tahadhari ingawa hajapeleka wanajeshi wengi eneo la Tigray. "Eritrea ina wanajeshi eneo la Tigray, lakini vita vinaendeshwa na wanajeshi wa Ethiopia," akasema.

Abdurahman anasema vita hivyo vinaendeshwa kutoka vituo vinne au sita. Maelfu ya wanajeshi wa Ethiopia na Eritrea waliwekwa katika vituo vilivyo karibu na mji wa Adigrat, eneo la Tigray. "Wako tayari kushambulia mji huo na mji mkuu wa Mekelle," akaeleza.

Duru zingine ziliambia BBC kuwa wanajeshi wa mataifa hayo mawili tayari wanasonga kutoka mji wa Shire kuelekea miji ya Aksum na Adwa. Ingawa mataifa ya kigeni yamekuwa yakitoa wito kwa pande mbili hasimu zikomeshe vita, Bw Abdurahman anasema huenda hilo lisifanyike.

"Kihistoria, matabaka ya watawala nchini Abyssinia, sasa Ethiopia, yamekuwa yakilinda na kutetea mamlaka yao. Walio na mamlaka makubwa hugeuka kuwa wafalme wa wafalme, hadi mtu mwingine aibuke. Hawana desturi ya kusuluhisha tofauti zao kwa amani," akasema Abdurahman.

Hata hivyo, Profesa De Waal alisema jamii ya kimataifa inafaa kuchukua hatua za haraka kukomesha vita hivyo. "Hatua hiyo isipochukuliwa kuna uwezekano wa kutokea mauaji ya halaiki huku idadi kubwa ya raia wakizongwa na njaa," akasema, akitaja matokeo ya utafiti uliofanywa Agosti ambao ulikadiria kuwa kati ya raia 385,000 na 600,000 walikufa katika vita hivyo jimbo la Tigray. Maafa hayo yalisababishwa na mapigano, njaa na ukosefu wa huduma za matibabu, miongoni mwa sababu nyingine.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ ALIVYOJIJENGA KUWA KIONGOZI ASIYEWEZA KUPINGWA

# KUPANDA KWA XI JINPING



*Miaka miwili baada ya kuingia mamlakani, serikali ilithibitisha kukamatwa kwa "duma", aliyekuwa mkuu wa usalama wa ndani Zhou Yongkang kwa ufisadi. Uchunguzi ulizua hofu kubwa ya kisiasa kwani ulikiuka kanuni kuwa wanachama wa Baraza Kuu la Kisiasa la Chama cha Kikomunisti China hawawezi kuabidhiwa kwa uhalifu*

• BEIJING

Si wengi waliobashiri kuwa Xi Jinping angekuwa kiongozi mwenye nguvu Zaidi China kwa miongo kadhaa - sasa anaelekea kuhudumu kwa muhula wa tatu kama rais.

Katika mwongo mmoja uliopita, si mengi yaliyojulikana kumhusu Xi, zaidi ya kuwa baba yake alikuwa mmoja wa viongozi walioongoza mapinduzi nchini humo. Historia ya kizazi chake ilimsaidia kuungwa mkono na wazee wa chama na kumwezesha kupanda ngazi kimamlaka ndani ya Chama cha Kikomunisti China (CCP), kwa sababu viongozi hao huwa na mamlaka ya kisiasa hata baada ya kustaafu. "Kabla ya kupandishwa cheo, Xi Jinping alichukuliwa kuwa mtu ambaye angeshawishiwa na kila mtu," akasema Joseph Fewsmithi, mtaalamu wa siasa za China katika Chuo Kikuu cha Boston. Lakini miaka 10 baadaye, uongozi wa Xi unaonekana kuwa usioweza kutikishwa. Ana mamlaka makuu kuliko watangalizi wake. Alifikia kiwango hiki namna gani?

**Mtutu wa bunduki**

Mao Zedong, mwanzilishi wa Taifa la Kikomunisti la Chama wakati mmoja alisema: "Mamlaka ya hupatikana kupitia mtutu wa bunduki."

Baada ya kuundwa kwa Jamhuri ya Watu

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Xi alivyozima wapinzani katika chama chake

Kutoka Uk 27

wa China mnamo 1949, Mao alihakikisha ilikuwa ni chama, wala si nchi, kilichosimamia Jeshi la Ukombozi (PLA). Tangu wakati huo, kiongozi wa CCP pia ameshikilia wadhifa wa Mwenyekiti wa Tume ya Kitaifa ya Jeshi China (CMC).

Xi alikuwa na bahati akilinganishwa na mtangulizi wake, Hu Jintao, kwa sababu alikuwa mwenyekiti cha CMC mara tu alipoingia mamlakani. Alichukua hatua ya haraka na kuzima upinzani ndani ya vikosi vya jeshi.

Tukio la kushangaza lilijiri miaka ya 2014 na 2015, Naibu Mwenyeti wa CMC Xu Caihou na aliyekuwa Jenerali wa PLA, Guo Boxiong walipokabiliwa na tuhuma za ufisadi. "Walistaafishwa baada ya kukabiliwa na tuhuma hizo. Lakini ujasiri wa Xi wa kulenga wawili hao ulipunguza ushawishi wa aliyekuwa kiongozi wa China Jiang Zemin katika jeshi la PLA," akasema Joel Wuthnow, ni afisa mkuu wa Chuo Kikuu cha Ulinzi wa Kitaifa (National Defense University).

"Hatua yake hiyo pia ilitoa ishara kwa maafisa wanaohudumu sasa kuwa hakuna anayepinga mamlaka ya Xi atakwepa shoka lake," akaongeza.

Mnamo 2015, Xi alifanya mabadiliko katika muundo wa jeshi. Alivunja vitengo vinne katika makao makuu ya jeshi, idara ya wafanyakazi, siasa, uchukuzi na silaha. Alibuni mashirika madogo 15 kuchukua nafasi ya vitengo hivyo.

Muundo huo mpya unawezesha CMC kutoa maagizo moja kwa moja kwa matawi mbalimbali ya jeshi - wakiwemo wakaguzi wa matumizi ya pesa ambao sasa wanawajibika moja kwa moja kwa CMC, anaongeza Bw Wuthnow.

Hii ndiyo maana kufikia sasa uaminifu kwa Xi unahimizwa nchini China.

Mwezi jana, "People Liberation Army Daily", gazeti rasmi la kijeshi nchini China, lilichapisha makala iliyokariri kuwa CMC ndiyo yenye usemi katika jeshi.

"Ujumbe huo unapinga uwezekano wa jeshi kuelekeza uaminifu wake kwa viongozi wakuu wa PLA ambao siku moja wanaweza kumpinga Xi," akasema Timothy Heath, mtafiti wa shirika la RAND lenye makao yake nchini Amerika. "Uaminifu kwa chama uliashiria kuwa PLA ilitarajiwa kutekeleza maagizo ya kuwezesha chama cha kikomunisti (CCP) na hasa Xi, kubakia mamlakani."



Wafuasi wapeperusha bendera za kitaifa na zile za Chama cha Kikomunisti huku wakitazama kufunguliwa kwa Kongamano la 20 la Chama cha Kikomunisti cha China mjini Huaibei, jimbo la Anhui, mashariki mwa China, mnamo Oktoba 16. Rais Xi Jinping alisifia China kuwa taifa lenye nguvu duniani na akataka umoja chini ya uongozi wake.

## Uaminifu kwanza

Xi pia amefaulu kuweka vyombo vyote vya usalama wa ndani chini ya udhibiti wake.

Miaka miwili baada ya Xi kuingia mamlakani, maafisa wa utawala walithibitisha kukamatwa kwa aliyekuwa mkuu wa usalama wa ndani Zhuo Yongkang kwa ufisadi. Yongkang alikuwa mshirika wa Bo Xilai, ambaye alikuwa mpinzani wa Xi.

Hatua hiyo ilizua hofu kubwa kisiasa kwani ilikiuka kanuni kwamba mwanachama wa Baraza Kuu la Kisiasa la Chama cha Kikomunisti China, asasi yenye mamlaka makuu, hawawezi kuadhibiwa kwa uhalifu. "Xi Jinping aligeuka kuwa mwanasiasa mwerevu ambaye alipanda ngazi ndani ya mfumo wa uongozi kabla ya kupata nafasi ya kuwa rais wa China," akasema Neil Thomas, mchanganuzi wa kisiasa wa shirika la Eurasia Group. "Viongozi wa chama cha kikomunistti waliounga mkono kupanda ngazi kwa Xi walishangaa jinsi alivyodhibiti mamlaka ndani ya muda mfupi," anaongeza.

Wachanganuzi wanasema kampeni ya Xi ya kupambana na ufisadi pia inatumika kuwazima washindani wake wa kisiasa na makundi mengine pinzani ndani ya chama tawala cha CCP.

Ndani ya miaka 10 iliyopita, watu Zaidi ya 4.7 milioni wamechunguzwa na asasi za kupambana na ufisadi. "Ndani ya miaka miwili iliyopita Xi pia aliwafuta kazi maafisa wa usalama waliomsaidia kupata mamlaka," akasema Victor Shih, mwanasayansi wa siasa katika Chuo Kikuu cha California. "Sasa asasi za usalama zinaendeshwa na maafisa waliofanya kazi na Xi miaka ya nyuma na ambao anawaamini," anaongeza Shih.

Xi pia ameweka washirika wake katika afisi za chama cha CCP katika miji ya Beijing, Shanghai na Chongquing, ambako wanahudumu kama makatibu.

Nyadhifa hizi ni muhimu kwa sababu wanaozishikilia wametwikwa wajibu wa kutafsiri na kutekeleza maamuzi ya chama katika miji hiyo yenye idadi kubwa ya wakazi," akasema Thomas.

Wakati huo huo, wanachama wote 281 wa kamati kuu katika mikoa walipandishwa vyeo na Xi," kulingana na data iliyokusanywa na Profesa Wu Guoguang wa Chuo Kikuu cha Victoria nchini Canada.

## Kuuda nembo yake kama mtu binafsi

Mnamo 2018, filosofia ya Xi kuhusu ujamaa iliwekwa katika katiba ya China. Hii ilisaidia kuweka kumbukumbu ya kiongozi huyu katika maisha ya raia na viongozi wa China. Filosofia ya Xi ililenga kuimarisha ukubalifu wa uongozi na mamlaka ya Xi kwa watu wote katika chama tawala, CCP na nchi kwa ujumla.

Ni sifa inaunganisha Xi, sio tu na Mao, bali pia viongozi wa China wa miaka iliyopita," anasema Profesa Jean-Pierre Cabestan anayehudumu katika Chuo Kikuu cha Hong Kong Baptist.

Vyuo vingi vikuu nchini China vimeanzisha vituo vingi vya utafiti kwa jina la Bw Xi, kulinganna na gazeti la Ming Pao linalochapishwa jijini Hong Kong. "Xi anamaamini kuwa falsafa na itikadi yake ni bora na kila mtu anapaswa kuikubali," anasema Profesa Andrew Nathan wa Chuo Kikuu cha Columbia.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ TRUSS ALIMTIMUA KWARTENG ILI KUOKOA KAZI YAKE

*Sunak alikuwa tayari kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, lakini wanachama wa chama cha Conservative hawakutaka kiongozi asiye Muingereza asili. Uongozi wa Truss sasa uko hatarini. Anaweza kuwa waziri mkuu wa nchi hiyo kuhudumu kwa muda mfupi zaidi*

# MSUKOSUKO UINGEREZA



**Waziri Mkuu wa Uingereza Liz Truss akitoka katika ofisi yake ya jijibni London kwenda katika Bunge kutangaza mpango wake wa bei ya kawi mnamo Septemba 8.**

● LONDON

Uthabiti haupatikani hapa, kuna msukosuko. Chama tawala Uingereza cha Conservative, mapema wiki jana kilikuwa kikitafuta kiongozi mpya, yaani waziri mkuu, karibu mwezi mmoja baada ya kujichagulia mmoja na wa nchi yao. Bi Liz Truss huenda akawa waziri mkuu wa Uingereza kuhudumu kwa muda mfupi sana.

Uingereza imekuwa na machansela wanne, ambao wadhifa wao ni kama wa waziri wa fedha, kwa kipindi cha miezi minne. Na kati ya Juni 2016, David Cameron alipojiuzulu kama waziri mkuu, na sasa, imekuwa na mawaziri wakuu watatu ilhali muhula kamili wa bunge huwa ni miaka mitano.

Mnamo Julai, Boris Johnson alilazimishwa kujiuzulu kama waziri mkuu mawaziri 50 na manaibu wao walipojiuzulu kutoka serikali yake kwa sababu ilikuwa imegubikwa na kashfa nyingi na hawakuzifichua.

Aliharibu zaidi kwa kuingia ofisi ya waziri mkuu ya Downing Street wakati ambao Uingereza ilikuwa imefungwa, na hivyo basi akavunja kanuni alizowekea kila mtu kuzuia kuenea kwa Covid-19.

Baadhi ya wabunge wa Conservative waliompigia kura Truss dhidi ya mpinzani wake Rishi Sunak wanataka aondoke ofisini chini ya mwezi mmoja tangu walipomchagua.

Cameron, aliyechaguliwa katika uchaguzi mkuu wa 2015 alipojiuzulu, chama cha Conservative kilifanya mashindano ya uongozi ambayo mshindi wake, Theresa May, alitwaa wadhifa wa Waziri Mkuu wa Uingereza.

Miaka mitatu baadaye May alipohindwa kuelewana na Ubelgiji kuhusu kujiondoa kwa Uingereza kutoka Muungano wa Ulaya, alipoteza imani bungeni na akajiuzulu. Uchaguzi ulifanywa na Johnson alishinda.

Katika uchaguzi wa Julai, tofauti kati ya Sunak na Truss kuhusu uchumi, kuelewa masuala, imani na kujieleza zilikuwa kubwa; Sunak alikuwa mbele sana ya Truss. Sunak, alielewa vyema suala muhimu la uchumi wakati wa mfumuko, akisema haukuwa wakati wa kuongeza ushuru. Truss alisema angepunguza ushuru.

Hata hivyo, wanachama 160,000 wanaopiga kura wa chama cha Conservative kati ya raia 70 milioni wa Uingereza walichagua Truss (wakati huo akiwa Waziri wa Mashauri ya Kigeni) badala ya Sunak (aliyekuwa Waziri wa Fedha) jinsi tu wabunge wao walivyokuwa wamefanya mwezi uliotangulia. Yalikuwa matokeo ya kushangaza kwa wengi wasio wanachama wa Conservative hasa waangalizi wasio raia wa Uingereza na wachanganuzi.

Kwa sababu Sunak ni PIO (Mtu Wa Asili ya Kihindi) na kwa sababu Truss ni Muingereza na mzungu na kwa sababu chama cha Conservative kimejaa wazungu, au 160,000 wanaopiga kura wengi wao ni wazungu, swali lililoibuka ni iwapo Conservative walikuwa tayari kwa kiongozi wa rangi ya Sunak, asiye Mwingereza asili.

Nchini India, ambako ugombeaji wa Sunak ulifuatiliwa kwa karibu, sio kwa sababu nchi hiyo kubwa ilikuwa koloni ya Uingereza, wachanganuzi kadhaa walitumia kauli mbiu yake sana. Kauli mbiu ya Sunak na hashtategi zilisema Tayari kwa Rishi na #Ready4Rishi mtawalia. Wachanganuzi wa India walifikia uamuzi kuwa, ingawa Sunak alikuwa tayari kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, Tories hawakuwa tayari kwa kiongozi asiye Mwingereza asili.

Wachanganuzi, wanachama wa Conservative na Bunge, sasa wanakubaliana na Sunak kuhusu uchumi kwa sababu Truss alipendekeza kupunguzwa kwa ushuru kwa kiwango kikubwa ambapo upungufu wa mapato utafadhiliwa kupitia ukopaji mkubwa (pauni 45 bilioni).

Hii ilishtua masoko, huku thamani ya pauni ikishuka, viwango vya kununua nyumba vikapanda na hazina za pensheni zikakumbwa na tishio la kuporomoka.

Msukosuko huo ulilazimisha Benki ya England, sawa na Benki Kuu, kuingilia kati na kununua bodi za serikali ambazo viwango vyake vya riba vinahusishwa na mfumuko ili kulinda hazina za pensheni kwa kuzipatia nafasi ya kuepuka kufilisika.

Hali hiyo ilipatia wabunge wa upinzani ujasiri wa kulaumu Conservative kwa kuharibu uchumi. Msukosuko huo ulilazimisha Truss kumfuta kazi waziri wake wa fedha, Kwesi Kwarteng, aliyekuwa akitekeleza sera zake na nafasi yake ikatwaliwa na Waziri wa Afya, Jeremy Hunt.

Hunt alibatilisha sera zote ambazo Kwarteng alikuwa ameanzisha kwa niaba ya Waziri Mkuu. Truss alimtimua Kwarteng ili kuokoa kazi yake, lakini sio wengi wanaofikiria atakuwa Waziri Mkuu kwa muda mrefu.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

**TANZIA**

■ PIA ALIHUDUMU KATIKA BODI ZA SHULE KADHAA

# MHUBIRI UPANGAJI UZAZI AONDOKA

*Waliopinga juhudi zake walisema alikuwa anawapotosha wapunguze idadi ya watoto waliokuwa nao huku kizazi chake kikizidi kunawiri*

● NA OSCAR OBONYO

Kenya ilipokuwa taifa la kwanza katika eneo la Afrika kusini mwa Sahara kukubali upangaji uzazi kama sera ya kitaifa, mwanamke mmoja alihamisha ujuzi wake wa ualimu kutoka darasani hadi jukwaa la umma.

Mnamo 1970, Salome Auma Wamalwa alianza kampeni ya kupigia debe upangaji uzazi katika eneo ambalo sasa linajulikana kama Kaunti ya Busia chini ya Shirika la Upangaji Uzazi Kenya (FPAK).

Kama alivyoungama baadaye kwa marafiki na familia, kazi hii ndiyo ilikuwa ngumu zaidi kuliko zote alizowahi kufanya maishani mwake. Changamoto kubwa ilitokana na kuwa alikuwa na watoto saba wazima na wajukuu waliozidi kuongezeka, jambo lililotumiwa na wakosoaji wake kupinga kampeni yake, wakisema anawapotosha wapunguze idadi ya watoto waliokuwa nao huku kizazi chake kikizidi kunawiri.

Kilikuwa kinaya kikubwa lakini ambacho hakikumtisha Salome. Alicheka shutuma hizo, akieleza kuwa alimakinika zaidi kuhakikisha watu wanapanga familia zao ili waweze kumudu vyema mahitaji ya watoto wao.

Salome aliaga dunia mnamo Oktoba 8, akiwa na umri wa miaka 81. Alikuwa na nafsi ya kipekee na bonge la mtu iliyekuwa rahisi kumuona kwenye umati au hafla. Wakazi wanakumbuka vyema miradi yake ya uhamasishaji: Alikuwa akisafiri kutoka eneo moja hadi lingine kwa pikipiki, kisha kutembea vijijini akiwa amevalia sare yake ya FPAK rangi ya kijani na manjano huku akihubiri injili ya kupanga familia.

Salome alikuwa mwendeshaji pikipiki wa kwanza mwanamke ambaye watu wamewahi kuona, na pikipiki yake ilikuwa aina ya kwanza kabisa ambayo watu wamewahi kuona. Kabla hajapata alikuwa na changamoto ya kuzunguka Wilaya nzima ya Busia. Alikuwa akiamka saa kumi alfajiri kila siku ili kuwahi basi la pekee lililopitia nyumbani alikoolewa katika kijiji cha Bukiri saa kumi unusu alfajiri.

Alipojiunga na FPAK mnamo 1971, Salome alikuwa mfanyakazi pekee aliyetumwa nyanjani katika wilaya hiyo yenye ukubwa wa kilomita 1,678 mraba, ambayo kwa sasa inajumuisha maeneobunge saba: Budalang'i, Butula, Funyula, Matayos, Nambale, Teso Kusini and Teso Kaskazini. Masaibu yake yalizidishwa na barabara mbovu na upungufu wa Matatu.

Hizi zilikuwa nyakati ngumu kwa mama huyo wa watoto saba, kama binti zake Nellie na Elizabeth wanavyokumbuka. Wakati mwingine angetembea masafa marefu ili kufika nyumbani baada ya kukosa gari, mara nyingi angenyeshewa na kurudi nyumbani kwa mume na watoto wake usiku. Kisha alilazimika kuketi chini na kuandika ripoti zake za nyanjani na kulala kwa saa chache tu kabla ya kurauka teka saa kumi alfajiri.

Si ajabu basi kuwa Salome alipewa pikipiki na mwajiri wake. Alijifunza kuiendesha katika muda wa siku nne. Lakini bado alikumbwa na changamoto nyingine nyanjani, kizingiti kikubwa zaidi kikiwa dhana potovu kuhusu upangaji wa familia.

Mwanzoni alikumbana na uhasama kutoka kwa wanaume, waliomshutumu kwa kutaka kuharibu familia zao. Baadhi yao waliamini kuwa upangaji uzazi ungewafanya wanawake kuwa viruka njia kwa kuwawezesha kufanya mapenzi na na wanaume wengine bila ushahidi wa mimba. Wengine walidai upangaji uzazi uliwafanya wanawake kuwa 'baridi' kitandani.

Ikizingatiwa kuwa Salome alikuwa mwanamke aliyezungumzia watu kuhusu masuala ya ngono, hatima ya kufeli ilionekana kumkodolea macho, lakini mwalimu huyo mcheshi wa zamani mwenye hulka ya kutaja mambo kinaga ubaga alishangaza wengi kwa ujasiri wake.

Profesa Julia Ojiambo, aliyekuwa Naibu Waziri Msaidizi katika Wizara ya Makao na Huduma za Jamii miaka ya 1980, Salome alipokuwa akiongoza kampeni hiyo Magharibi mwa Kenya, anamsifia kuwa mhudumu wa afya jasiri aliyeshinda itikadi potovu za kijinsia na kitamaduni ili kutoa huduma kwa jamii.

Upangaji familia ulikuwa katika kitengo cha Ojiambo, na anakumbuka kuwa kutaja tu "upangaji uzazi" ilikuwa mwiko katika jamii nyingi. Anamchukulia Salome kuwa mmoja wa wanajeshi wakakamavu nyanjani waliosaidia kuzika katika kaburi la sahau "dhana tele potovu" kuhusu suala hilo.

Aliporudi kutoka Colombo mnamo 1979, alikoongoza wajumbe wa Kenya kwa Kongamano la Kimataifa la Wabunge ambalo liliagiza mabunge yabuni sera mwafaka kuhusu idadi ya watu na maendeleo, Ojiambo anakumbuka Salome akimkumbatia na kumpongeza kwa kazi nzuri aliyofanya.

Kisadfa, Ojiambo alikuwa pia Mbunge wa Funyula, eneo ambako Salome alikuwa ametoka, lakini hawakukubaliana kisiasa. Salome aliegemea kambi ya aliyekuwa makamu wa rais Moody Awori, aliyemng'atua Ojiambo kama mbunge wa eneo hilo mnamo 1983.

"Dada yangu Salome alikuwa mshiriki mkuu wa maendeleo, lakini ilipohusu siasa, aliniambia wazi tulikuwa katika mikondo tofauti. Alikuwa mkweli na hakuwa na unafiki na nilimheshimu kwa hilo," Ojiambo akaambia Darubini ya Wiki.

Salome, ambaye alikuwa mtoto wa nane katika familia ya watu 14, aliolewa na Eli Augustine Namaindi, mtaalam wa kiuchumi aliyefariki Juni 2014. Salome alifunza katika shule kadhaa za msingi Kaunti za Busia, Mombasa, Nairobi na Kakamega kabla ya kujiunga na FPAK kama mhudumu wa jamii mnamo 1970. Baada ya kustaafu mnamo 1995, alihudumu katika bodi za shule kadhaa.

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*




**Salome Wamalwa alihubiri kuhusu upangaji uzazi.** PICHA | MAKTABA

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep








**SMS the word GAZETI to 20567,**

Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM